**Mbunge** CCM ajiuzulu kabla ya kula kiapo, chama chatoa kauli



UKURASA 3

**Kamati** kuchunguza chanzo cha moto kituo cha umeme Morogoro

UKURASA 7


Nipashe TESA
Jumanne Agosti 3, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Taifa linavyongoja kwa hamu uwekezaji 'huu' wa michezo
ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI
Unahitajika mjadala wa chakula kitaifa kukabili hofu na usalama
Ulishaji sumu, kemikali, vyakula feki

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Agosti 3, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580661

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Utouh aunga mkono wabunge kukatwa kodi

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride rasmi la Jeshi la Rwanda alipowasili Ikulu Kigali nchini Rwanda jana, ikiwa ni ziara ya kiserikali ya siku mbili kwa mwaliko wa Rais Paul Kagame. **PICHA: IKULU**

## Tanzania, Rwanda zaafikiana mambo 10

UKURASA 3

# IGP aionya CHADEMA maandamano



**ATANGAZA** operesheni bodaboda, Kibiti... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA ZAKIMBIZANA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Utouh aunga mkono wabunge kukatwa kodi

**Na Maulid Mmbaga**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, amesema anaunga mkono hoja ya Mbunge wa Ukonga, Jerry Slaa na Hussein Bashe, kuhusu wabunge kukatwa kodi.

Akizungumza jana katika mahojiano na kituo kimoja cha runinga, alisema miongoni mwa misingi mikubwa ya kodi ni usawa kwa kuwa kodi yoyote haitakiwi kuwa na matabaka ya watu.

"Tunalipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi sasa hawa wabunge si wana kipato, wanapokea mshahara kwanini wasilipe kodi, mantiki ya hiyo haipo," alihoji Utouh.

Julai 23, Mbunge wa Ukonga, Slaa, akihutubia wananchi katika jimbo hilo, alisema imefika hatua wabunge waanze kulipa kodi kupitia mishahara yao ili wapate uwezo wa kuwaambia wananchi na wao walipe kodi.

Pia Utouh alizungumzia nafasi ya CAG aliyowahi kuihudumia miaka kadhaa iliyopita kuwa nafasi hiyo ni nyeti na inamtaka mtu kuwa muadilifu ili kutende haki kwa sababu inabeba dhamana ya wananchi.

"Madhumuni ya ukaguzi ni kuleta maboresho, serikali ifanye vizuri zaidi kwahiyo mkaguzi ni mshauri mkuu wa serikali katika kuweka mambo sawa ili fedha na rasilimali za wananchi zitumike vizuri kwa maendeleo jamii.

"Mwaka 2012 baada ya ripoti yangu kutoka mawaziri wanane waliachia ngazi, kwasababu ya ile ripoti ilileta mtafaruku watu wakawa wanamwongelea CAG Utouh, lakini anayoyaripoti sio ya kwakwe ni vitu anavyokwenda kuviona katika ukaguzi wake," alisisitiza Utouh.

Alisema yeye hakuwatoa mawaziri, lakini kwasababu ripoti yake ilianika yale yaliyokuwa ya ukweli, ndiyo iliwalazimisha kuwajibishwa.

Alibainisha kuwa mwaka 2007-8 vyama vya siasa vilikuwa vinatumia zaidi ripoti ya CAG kuichambua serikali, na ikafika mahali akashauri kuwa chama tawala kiachie vyama vya upinzani vitumie ripoti ya CAG kuikosoa serikali.

"Ilifika kipindi tukasikia mawaziri mizigo, ilikuja baada ya majadiliano, na chama tawala kikaanza kuitumia ripoti ya CAG kuikosoa serikali ambayo ni serikali yake, na hiyo ndiyo imekuwa kama utamaduni sasa," alisema Utouh.

Pia alisema ripoti ya CAG haiandaliwi kwa ajili ya kumnufaisha mtu, inaandaliwa kwa dhumuni la kuweka bayana hali iliyopo ya utendaji wa serikali.

Alisema chama tawala kina wajibu wa kuisimamia serikali yake na kuhakikisha inatekeleza yale yaliyokisababisha chama kichaguliwa kuingia madarakani.

"Serikali yoyote inayokumbatia ufisadi na matumizi mabaya ya rasilimali za umma kwa kipindi kirefu haidumu itaanguka kwasababu wananchi hawataikubali.

Katika uchambuzi wa watu wanaopewa nafasi ya kusimamia rasilimali za nchi kuwe na uangalizi zaidi, je hawa tunaowapeleka wana maadili ya kufanya ile kazi, wana uwezo na ujuzi, ili majukumu wanayopatiwa wakayatimize kwa weledi," alishauri Utouh.

Alisema uteuzi wowote mtu anaopata wa utumishi wa umma, anapaswa kujua kuwa hiyo ni dhamana aliyopewa inayomfanya awe mtumishi wa watu na si vinginevyo, kwa kuwa kuna baadhi ya watu wakishapata nafasi wanajiona wako juu, na hiyo ndiyo inaleta matatizo.

## Mama Majaliwa aongoza wake wa wastaafu chanjo

**Na Hellen Mwango**

MKE wa Waziri Mkuu, Mary Majaliwa, jana aliwaongoza wake wa mawaziri wakuu wastaafu, wahariri wa vyombo vya habari na waandishi kuchoma chanjo ya virusi vya corona.

Uchomaji wa chanjo hiyo aina ya Johnson Johnson ulifanyika katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wakazi mbalimbali wa Jiji hilo.

Viongozi wengine waliohudhuriwa ni pamoja na Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Tunu Pinda, Mke wa Waziri Mkuu mstaafu Rashidi Mfaume Kawawa, Hasna Kawawa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupata chanjo hiyo, Mary Majaliwa, alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwaletea Watanzania chanjo hiyo na kwamba Watanzania wajitokeze kwa wingi kupata chanjo.

Mama Majaliwa alisema: "Namshukuru Rais Samia kwa kutuletea chanjo hii, nami naungana na wahariri na waandishi wa habari kupata chanjo leo," alisema Mama Majaliwa.

Mjumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), ambaye ni Katibu Tawala wa Halmashauri ya Handeni, Mashaka Mgeta, alisema ameungana na wanahabari wenzake kupata chanjo na kwamba Watanzania waungane na serikali katika kupata chanjo hiyo.

Mgeta alisema: "Watanzania wajitokeze na mara itakapopelekwa Wilaya ya Handeni, nawashauri wajitokeze kupata chanjo hii, mimi tayari nimeshachanja."




Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, IGP Simon Sirro, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuimarika kwa hali ya usalama hapa nchini na kuwataka wananchi kuendelea kudumisha amani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# IGP Sirro awaonya CHADEMA, bodaboda

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, amepiga marufuku wanachama wa Chama cha Demokrasia na Mendeleo (CHADEMA) kufanya maandamano na mikusanyiko katika eneo la mahakama, huku akisisitiza kuwa kwa yeyote atakayekiuka atawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Alitoa onyo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari pamoja na mambo mengine aliwataka wananchi waliopanga kufanya maandamano katika mahakama waache kwani mahakama ni sehemu nyeti ambayo hairuhusiwi kujazana.

Kamanda Sirro alitoa onyo hilo baada ya Julai 31, mwaka huu Katibu Mkuu CHADEMA, John Mnyika, kuwataka wanachama wote ndani na nje ya Mkoa wa Dar es Salaam kujitokeza katika Mahakama ya Kisutu siku ambayo kesi ya Mbowe itatajwa.

Kamanda Sirro alisema suala la vyama vya siasa, viongozi wa dini na mashirika ya kibinafsi kusema kuwa Mwenyejiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe ameonewa si sahihi, hivyo wasubiri mahakama itimize wajibu wake na ndiyo itakayoamua kuwa ni mhalifu ama laa.

"Suala la wanachama wa chama hicho kusema kuwa watafanya maandamano, wanavunja sheria na watakapofanya hivyo wasije wakalaumu jeshi, utakapoandamana utakuwa ni mhalifu, utakapovunja sheria polisi wala Sirro hatakuacha," alisema IGP Sirro.

Aliongeza: "Sisi hatufanyi siasa, kazi yetu ni kuhakikisha kuwa amani na utulivu inakuwapo, kama kikundi cha watu wachache kwa sababu ya kutopata nafasi ya madaraka ya kisiasa na wanafikiri wanaweza kupata nafasi ya kutuvuruga haipo, niwaombe Watanzania tuache wale watu wachache wanaotaka kupambana na serikali wapambane nayo kwa sababu labda wanasababu zao," alisema Sirro.

Kamanda Sirro alisema mahakama ni sawa na kituo cha polisi, hivyo mtu yeyote akitaka kuvamia mahakama au kituo cha polisi atakung'utwa kwa mujibu wa sheria.

**OPERESHENI KIBITI**

Kamanda Sirro alisema operesheni Kibiti imerudi rasmi na wameweka askari katika Wilaya ya Kibiti, huku akitoa wito kwa wananchi wa eneo hilo kutoa ushirikiano kwa polisi endapo wataona hali yoyote wasiyoielewa, kwamba wasisubiri matukio ya kipindi cha nyuma.

Pia aligusia suala la ulinzi shirikishi kuwa kumekuwa na changamoto katika uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi.

Alisema wenyeviti wa serikali za mitaa kwa mujibu wa sheria za halmashauri wanawajibika katika suala zima la ulinzi na usalama kwenye mitaa, lakini kuna watu ambao hawataki kushiriki katika kulinda au kuwachangia wale wanaofanya ulinzi.

**OPERESHENI BODABODA**

Kamanda Sirro alisema Jeshi la Polisi kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia sasa itaendesha operesheni kamata madareva bodaboda ambao wanavunja sheria barabarani.

Alisema ajali za bodaboda zimekuwa nyingi zinazosababishwa na wao wenyewe kutofuata sheria za barabarani ikiwamo kutokuvaa kofia ngumu.

"Tumetoa maelekezo kwa makamanda wote nchi nzima wahakikishe wanafanya operesheni ya mwezi mzima kupambana na hawa bodaboda wasiofuata sheria za usalama barabarani," alisema IGP Sirro.

## HABARI KITAIFA



Mshindi wa zawadi kubwa ya Kampeni ya Twende Mjini na M-Pesa ya Vodacom Tanzania PLC, Neema Ikolo, akiwa kwenye gari lake alilokabidhiwa baada ya kutangazwa mshindi katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Vodacom iliendesha kampeni hii kwa wiki nane kwa lengo ya uhamasisha wateja wake kutumia huduma za kidijitali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania, Rwanda zakubaliana mambo 10

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA na Rwanda, zimekubaliana kuimarisha zaidi ushirikiano wao katika mambo 10.

Marais wa nchi hizo, Samia Suluhu Hassan wa Tanzania na Paul Kagame wa Rwanda walikubaliana mambo hayo jana nchini Rwanda.

Viongozi hao walifanya makubaliano hayo jana baada ya Rais Samia kuanza ziara ya kikazi ya siku mbili nchini humo na anatarajia kuikamilisha ziara leo.

Miongoni mwa mambo waliyokubaliana ni ushirikiano wa kiuchumi na kisiasa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Jambo jingine ni kuimarisha zaidi ushirikiano katika shughuli za biashara, uwekezaji ambazo zitanufaisha pande zote hizo mbili.

Mengine waliyokubaliana ni katika kuboresha masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

"Kama mnavyojua, Tanzania tuna mkongo ambao tumeusambaza katika nchi jirani na pia Rwanda wanatumia, na leo tumesaini makubalinao kwamba tuweke nguvu zaidi kwenye uhusiano mzuri wa matumizi hayo ya TEHAMA," alisema Rais Samia.

Jambo jingine ambalo walikubaliana kushirikiana ni katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

"Kuhusu ugonjwa wa corona, tumezungumza kwa mapana yake, tumeweka mikakati ya kushirikiana kupitia kituo chetu cha Rusumo, lakini kupitia kushirikiana katika mambo ya dawa na mambo mengine," alisema Rais Samia.

Kwa upande wake Rais Kagame alisema mambo mengine ambayo wamekubaliana ni kushirikiana zaidi katika kuboresha masuala ya miundombinu ikiwamo reli ya kisasa (SGR), huduma za bandari, uzalishaji wa maziwa pamoja ushirikiano wa kufanya kazi pamoja.

"Tunaamini kwamba makubaliano haya yatazidi kudumisha zaidi udungu na ushirikiano uliopo katika nchi zetu hizi mbili," alisema Rais Kagame.

"Tumekubaliana pia kwamba tunahitaji pia nguvu ya ziada katika kupambana na ugonjwa huu wa Covid-19, tumepanga kufanya kazi kwa karibu sana na ndugu zetu Watanzania katika kupambana na janga hili, kipekee nimeshukuru sana kutembelewa na Rais Samia na ninaamini haya tuliyokubaliana yatakuwa na manufaa makubwa sana kwa nchi zetu hizi na nje ya nchi zetu."

Katika mazungumzo yake, Rais Samia alitoa salamu za pole kwa nchi hiyo kutokana na janga lililowakumba la tetemeko la ardhi.

Pia alimshukuru Rais Kagame kwa ushirikiano ambao nchi hiyo iliutoa katika kipindi walichoondokewa na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

# Mbunge wa CCM ajiuzulu kabla ya kuapa

**Na Beatrice Shayo**

MBUNGE wa Jimbo la Konde (CCM), Sheha Mpemba Faki, ameandika barua ya kujiuzulu, kwa akichokieleza kuwa ni kutokana na changamoto za kifamilia.

Mbunge huyo alifanya uamuzi huo jana, kabla ya kuapishwa baada ya kushinda kwenye uchaguzi mdogo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, wamepokea kwa masikitiko barua ya kujiuzulu kwa mbunge huyo.

"Katika barua yake Mheshimiwa Sheha Mpemba Faki, ameeleza kwamba amefikia uamuzi huo kutokana na changamoto za kifamilia, jambo ambalo chama hakina uwezo wa kumzuia hasa ikizingatiwa kwamba ni haki yake ya msingi kama ilivyo kwa haki ya kuomba ridhaa ya kugombea nafasi ndani ya CCM," alisema Shaka.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa CCM inawaomba wanachama wote kuwa watulivu katika kipindi hiki wakati wakisubiri taratibu nyingine.

Julai 18, mwaka huu ulifanyika uchaguzi mdogo katika Jimbo la Konde kutokana na kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Khatib Said, Mei 19, mwaka huu.

Matokeo ya uchaguzi huo yalitangazwa Julai 19, 2021, Faki alipata kura 1,796 kati ya kura halali 5,020 zilizopigwa.

# Mbowe akimbilia Mahakama Kuu

**Na Kulwa Mzee**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kupitia Wakili wake Peter Kibatala, amewasilisha maombi Mahakama Kuu akitaka itamke kwamba kuna ukiukwaji wa haki zake za kikatiba katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Mbowe amefungua maombi dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akidai wamevunja haki zake kikatiba kwa kushindwa kumpa nafasi ya kusikilizwa kikamilifu.

Maombi ya Mbowe yaliwasilishwa jana akilalamikia kuvunjwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu Uchumi ambayo ameshtakiwa nayo kwa makosa ya ugaidi.

Wakili Kibatala amedai kwa mujibu wa sheria hizo mtuhumiwa anataka asishikiliwe zaidi ya saa 48 kituo cha polisi na akifikishwa mahakamani hakimu anatakiwa kuhakikisha kaelewa mashtaka yanayomkabili.

Amedai Mbowe ameshikiliwa Oysterbay tangu Julai 21, mwaka huu hadi Julai 26 alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa ugaidi.

Katika maombi hayo anadai sheria zimevunjwa, mteja wake alikaa kituoni zaidi ya saa 48, alilazwa sakafuni bila kujali usalama wa afya yake, wamevunja haki zake za kikatiba, wamemtesa na kumdhalilisha.

Polisi wanadaiwa kuvunja haki hizo kwa kushindwa kumpa nafasi ya kumsikiliza kikamilifu, na walishindwa kutoa taarifa kwa mawakili wake ama ndugu yake wa karibu.

Alidai Mbowe alipelekwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, bila kuambiwa anakwenda wapi na alipopanda kizimbani mahakama ilikiuka haki za kikatiba kwa kushindwa kumuuliza kama kaelewa mashtaka yanayomkabili.

"Alitakiwa afahamishwe mashtaka yake kiufasaha, mashtaka mazito, mahakama haijamuuliza kaelewa ama la zaidi ya kumwambia haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo," alidai Kibatala katika maombi yake.

Pia alidai Mbowe hakupewa hati ya mashtaka hadi Julai 27, mwaka huu mawakili wake walipokwenda nayo gerezani.

"Tunaomba mahakama itamke kuna upungufu na haki za Mbowe zimekiukwa," alidai Kibatala.

Mbowe alipanda kizimbani na kusomewa mashtaka na Wakili Esther Martin akidaiwa kati ya Mei na Agosti mwaka jana katika Hoteli ya Aishi pamoja na wenzake walikula njama ya kutenda kosa.

Katika shtaka la pili anadaiwa katika tarehe hizo mshtakiwa Mbowe alitoa fedha kwa ajili ya kufadhili vitendo vya ugaidi.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu lolote sababu mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza shauri hilo, alipelekwa gerezani hadi Agosti 5, mwaka huu, atakapounganishwa na washtakiwa wengine katika kesi namba 63 ya mwaka 2020.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **ADILI AUCTION MART, WAUNGWANA AUCTION MART, MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED, COPS AUCTIONMART AND COURT BROKERS, NSOMBO AUCTION MART** kwa niaba ya Access Microfinance Bank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KIJITONYAMA | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | MASARE/S,ZAINABU | MASARE/S,ZAINABU | NYUMBA | KIBAMBA KWA MANGI | 18/08/2021 |
| 2 | KIJITONYAMA | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | HUSSENI/ADANI, TWALIBU | HUSSENI/ADANI,TWALIBU | NYUMBA | KKIMARA TEMBONI | 18/08/2021 |
| 3 | KIJITONYAMA | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | KANJE/CLAUDY,LILIAN | KANJE/CLAUDY,LILIAN | NYUMBA | MABIBO FARASI | 18/08/2021 |
| 4 | MBEYA | ADILI AUCTION MART LIMITED | LAINI/G,PETRO | LAINI/G,PETRO | NYUMBA | MBEYA | 18/8/2021 |
| 5 | MBEYA | ADILI AUCTION MART LIMITED | LAINI/G,PETRO | MATAMBA/PETRO,EDWINI | GARI | MBEYA | 10/08/2021 |
| 6 | MBEYA | ADILI AUCTION MART LIMITED | MWAIKAMBO/B,ALVALES | MWAIKAMBO/N,BENARD | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 35957-MBYLR | KYELA | 18/08/2021 |
| 7 | MBEYA | ADILI AUCTION MART LIMITED | MWAKISOLE/A,ANANGISYE | MWAKISOLE/A,ANANGISYE | NYUMBA YENYE HATI YA KIMILA NAMBA 98RNG/4420 | TUKUYU | 18/08/2021 |
| 8 | MBEYA | ADILI AUCTION MART LIMITED | LUPONDO/SAMOJA,RODRICK | LUPONDO/SAMOJA,RODRICK | NYUMBA | KYELA | 18/08/2021 |
| 9 | MBEYA | ADILI AUCTION MART LIMITED | MWAKYAMBIKI/M,MPELIGWA | MWAKYAMBIKI/M,MPELIGWA | NYUMBA YENYE HATI No. 35681,35684 NA 41457 -MBYLR | KYELA | 18/08/2021 |
| 10 | KIJITONYAMA | COPS AUCTION MART AND COURT BROKERS | PALANJOI/N,PERIS | MWANG'ONDA/E,MAGRETH | NYUMBA | NYAMBWERA-TANDIKA | 19/08/2021 |
| 11 | KIJITONYAMA | NSOMBO AUCTION MART | KAWISHE/HABART,PRISCUS | KAWISHE/HABART,PRISCUS | KIWANJA | MAKABE MPAKANI | 19/08/2021 |
| 12 | KUJITONYAMA | WAUNGWANA AUCTION MART | SANGA/LAMECK,JOVIN | SANGA/LAMECK,JOVIN | VIWANJA 2 | BANGULO NA CHANIKA | 19/08/2021 |
| 13 | KIJITONYAMA | COPS AUCTION MART AND COURT BROKERS | ISSEME/MALABA,FREDY | KOMBA/NATHAN,GRACE | NYUMBA | MBAGALA ZOMBOKO | 19/08/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa.
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa.

**MAWASILIANO**
**MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED - 0755506970**
**ADILI AUCTION MART - 0767873988, WAUNGWANA AUCTION MART - 0713077474**
**COPS AUCTION MART AND COURT BROKERS - 0716884999, NSOMBO AUCTION MART - 0712055623**
**WOTE MNAKARIBISHWA**

216389102

## HABARI KITAIFA

# Mkimbizi mbaroni kwa madai uhalifu wa silaha

**Na Pendo Thomas,**

KIGOMA

JESHI la Polisi mkoani Kigoma linamshikilia mkimbizi mmoja kutoka katika Kambi ya Nduta mkoani Kigoma, Sabushimike Abraham (33), kwa tuhuma za kutekeleza uhalifu wa kutumia silaha ikiwamo kuteka magari na uvamizi majumbani.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema Julai 30, mwaka huu, walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo.

Kamanda Manyama ameeleza mnamo Julai 30 mwezi uliopita walifanikiwa kumkamata mtu huyo ambaye ni mkimbizi, akituhumiwa kutekeleza uhalifu katika Wilaya ya Kasulu na Kibondo.

Alisema katika mahojiano na mtuhumiwa huyo alitoa taarifa ya kuwa ana silaha aliyoificha katika Kijiji cha Busunzu wilayani Kibondo, baada ya polisi kufika katika eneo hilo kukuta bunduki aina ya AK 47 ikiwa na magazine mbili na risasi 176.

Kamanda Manyama alisema katika tukio lingine watu wawili katika eneo la Karya waliokuwa wakijihusisha na uporaji wa pikipiki wameuawa na wananchi wenye hasira, baada ya kutekeleza tukio la kumkodi mwendesha pikipiki kisha kumjeruhi kwa kumkata kwa mapanga na kuondoka na pikipiki.

Alieleza baada ya taarifa kuenea walizingirwa na wananchi na kwa nyakati tofauti waliwashika na kuwaua huku Jeshi la Polisi likimshikilia mtu mmoja aitwaye Isack Paulo kutoka Sumbawanga ambaye ni mmoja wa waliokuwa wakihusika na wizi huo.

Kamanda Manyama alitoa rai kwa wananchi pindi wanapotoa ushirikiano wa kuwakamata wahalifu wasiwaue ili kuwezesha hatua zingine zaidi kuchukuliwa.




Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara (TCB), Sabasaba Moshingi (wapili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani (wapili kushoto), wakisaini mikataba ya makubaliano na ushirikiano wa kuwapatia huduma za kifedha wateja wa benki hizo, wakati wa uzinduzi uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Miamala wa Benki ya Standard Chartered, Efeh Amoh, na kulia ni Mkurugenzi wa Teknolojia na Uwendeshaji wa TCB, Jema Msuya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia ateua wakurugenzi halmashauri

**Elizabeth Zaya na Mary Geogrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya 184 huku baadhi wakihamishwa vituo vyao vya awali na wengine wakichaguliwa wapya kujaza nafasi zilizokuwa zimeachwa wazi.

Baadhi ya wakurugenzi waliohamishwa vituo ni pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda ambaye anakwenda Karagwe, Michael Nzyungu, mwingine ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Spora Liana anayekwenda Jiji la Tanga.

Walioteuliwa Mkoa wa Arusha

Walioteuliwa kwenda katika Mkoa wa Arusha ni pamoja na Dk. John Pima(Jiji la Arusha), Zainabu Makwinya (Meru), Seleman Msumi (Arusha), Juma Mhina (Ngorongoro), Stephen Anderson (Longido), Raphael Siumbu (Monduli) na Karia Rajabu (Karatu).

**DAR ES SALAAM**

Walioteuliwa ni Elasto Kiwale (Kigamboni), Beatrice Kwai (Ubungo), Jumanne Shauri (Jiji la Ilala), Hanifa Hamza (Kinondoni) na Elihuruma Mabelya (Temeke).

**DODOMA**

Walioteuliwa ni Yusuph Semwaiko (Wilaya ya Kondoa), Paul Sweya (Kondoa Mji), Siwema Juma (Chemba), Athumani Masasi (Bahi), Dk. Semistatusa Mashimba(Chamwino), Dk. Omary Nkulo (Kongwa), Mwanahamisi Ally (Mpwapwa) na Joseph Mafuru (Jiji la Dodoma).

**GEITA**

Walioteuliwa ni Lutengano Mwaliba (Bukombe), Saada Mwaruka (Mbogwe), Mandia Kihiyo (Chato), Husna Chambo (Nyang`wale), John Wanga (Gaita) na Zainabu Michuzi (Mji wa Geita).

**IRINGA**

Walioteuliwa ni Bernard Limbe (Manispa ya Iringa), Bashiri Mhoja (Iringa), Happiness Laizer (Mafinga), Lain Kamendu (Kilolo), Zaina Mlawa (Mufindi).

**KAGERA**

Walioteuliwa ni Innocent Mukandala (Biharamulo), Hamid Njovu (Bukoba), Fatina Laay (Bukoba), Elias Kayandabila (Muleba), Waziri Kombo (Misenyi), Solomon Kimilike (Ngara), Michael Nzyungu (Karagwe) na Sael John (Kyerwa).

**KATAVI**

Walioteuliwa ni Sophia Kambuli (Mpanda), Mohammed Ntandu (Msimbo) Catherine Mashalla (Mpimbwe), Teresia Irafay (Mlele) na Shaban Juma (Tanganyika).

**KIGOMA**

Walioteuliwa ni Joseph Rwiza (Kasulu), Dollar Kusenge (Mji Kasulu), Ndaki Mhuli (Kakonko), Rose Manumba (Kigoma), Deocles Murushwagire (Kibondo), Zainabu Mbunda (Uvinza), Essau Ngoloka (Buhigwe) na Athumani Msabila (Kigoma Ujiji).

**KILIMANJARO**

Walioteuliwa ni Kastori Msigala (Moshi), Godwin Chacha (Rombo), Annastazia Tutuba (Same), Upendo Mangali (Siha), Dionis Myinga (Hai), Mwajuma Nasombe (Mwanga) na Dk. Rashid Gembe (Manispaa ya Moshi).

**LINDI**

Walioteuliwa ni George Mbilinyi (Mtama), Juma Mwele (Lindi), Eston Ngillangwa (Kilwa), Tina Sekambo (Liwale), Chionda Mfaume (Nachingwea) na Frank Chonya (Ruangwa).

**MANYARA**

Walioteuliwa ni Samweli Gunza (Simanjiro), John Nchimbi (Kiteto), Anna Mbogo (Babati), Yered Myenzi (Mji Mbulu), Jenifa Omolo (Hanang`), Dk. Zuwena Kondo (Mji Babati) na Abubakar Kuuli (Mbulu).

**MARA**

Walioteuliwa ni Emmanuel Mkongo (Bunda), Francis Namaumbo (Rorya), Pamela Msongela (Musoma), Gimbana Ntavyu (Mji Tarime), Bosco Ndunguru (Musoma), Patricia John (Butiama), Solomon Shati (Tarime), Changwa Mkwazu (Bunda) na Kivuma Msangi (Serengeti).

**MBEYA**

Walioteuliwa ni Stopho Katemba (Mbeya), Amedo Ngwadidako (Jiji Mbeya), Ezekiel Magehema (Kyela), Missana Kwangura (Mbarali), Tamim Kambona (Chunya), Loema Isaaya (Busokelo) na Renatus Mchau (Rungwe).

**MOROGORO**

Walioteuliwa ni Saida Mahungu (Ulanga), Stephen Kaliwa (Mlimba), Lena Nkaya (Ifakara), Hassan Njama (Mvomero), Kibena Mabuha (Kilosa), Rehema Bwasi (Morogoro), Asajile Mwambambale (Gairo), Joanifaith Kataraia (Malinyi) na Ally Machela (Manispaa Morogoro).

**MTWARA**

Walioteuliwa Emmanuel Mwaigoboko (Mtwara), Thomas Mwailafu (Nanyamba), Erica Yegella (Mtwara), Duncan Thebas (Newala), Apoo Tindwa (Masasi), Shamim Mwariko (Mji Newala), Ibrahim Mwanauta (Wilaya Nanyamba), na Mussa Gama (Tandahimba).

**MWANZA**

Walioteuliwa ni Modestus Apolinary (Ilemela), Lutengano Mwaliba (Misungwi), Emmanuel Sherembi (Ukerewe), Fidelica Myuvela (Magu), Selemani Yahya (Jiji la Mwanza), Binuru Shekidele (Sengerema), Paulo Malaga (Buchosa), Happiness Msanga (Kwimba).

**NJOMBE**

Walioteuliwa ni Dollar Kusenge (Mji wa Njombe), Sunday Ndori (Ludewa), William Makufwe (Makete), Keneth Keneth (Makambako), Maryam Muhaji (Wanging`ombe) na Sharifa Nabarang`anya (Njombe).

**PWANI**

Walioteuliwa ni Mshainu Munde (Mji Kibaha), Kuruthum Ammour (Chalinze), Hanan Mohamed (Kisarawe), Mwantum Mgonja (Mkuranga), Butamo Ndalahwa (Kibaha), Shauri Selenda (Bagamoyo), Mohamed Mavura (Kibiti), Kassim Ndumbo (Mafia) na John Kayombo (Rufiji).

**RUKWA**

Walioteuliwa ni Jacob Mtalitinya (Manispaa Sumbawanga), William Anyitike (Nkasi), Shafti Mpenda (Kalambo) na Lightness Msemo (Sumbawanga).

**RUVUMA**

Walioteuliwa ni Fredrick Sagamiko (Manispaa Songea), Neema Maghembe (Songea), Sajidu Mohamed (Madaba), Chiriku Hamisi (Namtumbo), Jimason Mhagama (Nyasa), Chiza Marando (Tunduru), Grace Stephen (Mji Mbinga) na Juma Haji (Mbinga).

**SHINYANGA**

Walioteuliwa ni Nice Munisy (Shinyanga), Anderson Msumba (Mji Kahama), Charles Fussi (Msalala), Lino Mwageni (Ushetu), Emmanuel Johson (Kishapu na Jomary Satura (Manispaa Shinyanga).

**SIMIYU**

Walioteuliwa ni Simon Berege (Maswa), Adrian Jungu (Mji Bariadi), Elizateh Matias (Itilima), Halid Mbwana (Bariadi), Veronica Vicent (Busema) na Maolen Dakawa (Meatu).

**SINGIDA**

Walioteuliwa ni Ester Chaula (Singida), Michael Matomora (Iramba), Justine Kijazi (Ikungi), Melkizedek Humbe (Manyoni), John Mgagulwa (Itigi), Zeflin Lubuva (Manispaa Singida) na Asia Mosses (Mkalama).

**SONGWE**

Walioteuliwa ni Cecilia Kavishe (Songwe), Philimoni Magesa (Tunduma), Regina Beida (Momba), Abdallah Nandonde (Mbozi) na Geofrey Nnauye (Ileje).

**TABORA**

Walioteuliwa ni Shomary Mndolwa (Mji Nzega), Kiomoni Kibamba (Nzega), Baraka Zikatimu (Urambo), Dk. Peter Nyanja (Manispaa Tabora), Hemed Magaro (Uyui), Jerry Mwaga (Kaliua), Selemani Pandawe (Sikunge), na Fatuma Omary (Igunga).

**TANGA**

Walioteuliwa ni Gracia Makota (Kilindi), Ikupa Harrison (Lushoto), George Haule (Bumbuli), Nasib Mmbaga (Muheza), Isaya Mugishangwe (Pangani), Zahara Msangi (Mkinga), Saitoti Stephen (Handeni), Nicodemus John (Korogwe), Spora Liana (Jiji la Tanga) na Halfan Magani (Korogwe).

Aidha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amewataka wakurugenzi wawili ambao majina yao yamejirudia katika nafasi mbili za uteuzi, waripoti katika eneo ambalo jina limetokea kwa mara ya kwanza.

Alisema wateuliwa wote wanatakiwa kuripoti vituo vya kazi leo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maparachichi yahitaji soko

**SERIKALI** mara kadhaa imekuwa ikihamasisha kilimo cha parachichi kwamba ni fursa kwa wakulima, na kwamba zao hilo linaweza kuwatoa kimaisha.

Zao hili linastawi kwa wingi katika mikoa yenye hali ya hewa ya baridi, ingawa wananchi wengi wa maeneo hayo hawajaiona fursa hiyo, pengine kutojua kuwa lina soko ndani na nje ya Tanzania. Takribani miaka miwili iliyopita, serikali ilianza kusisitiza kwa bidii uzalishaji wake pamoja na kuahidi kuwatafutia soko la ughaibuni wakulima, hususani mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Sasa serikali inasema moja ya mikakati yake kwa wakulima wa maparachichi, ni kuendelea na mazungumzo na serikali ya Afrika Kusini ili kupata soko la matunda hayo yanayolimwa katika maeneo mbalimbali nchini. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema juzi akiwa mkoani Mbeya kwamba, hatua hizo zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zitasaidia kutatua kero ya wananchi kuingia hasara kwa kutupa matunda hayo baada ya kuoza, kutokana na kukosa soko.

Alisema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Rungwe baada ya kutembelea mashamba ya kiwanda cha maparachichi cha Kampuni ya Kuza Afrika Ltd kilichopo katika Kijiji cha Ilolo, Kata ya Kiwira.

Pamoja na ufafanuzi huo, anawataka wananchi wa wilaya hiyo na maeneo mengine ambayo zao hilo linastawi, kuendelea kuzalisha kwa wingi kuwa soko hilo ni la uhakika na litapatikana.

Lakini alisema, Wizara ya Kilimo imepewa kazi ya kusimamia kilimo cha maparachichi na kuwatafutia wakulima mbegu bora, kutunza miche shambani na kutafuta masoko na kuwataka wakulima walime kwa nguvu. Aidha, aliwaagiza maofisa kilimo kuanzia wa mkoa mpaka wilaya kuhakikisha wanawasaidia wakulima kulima kisasa zao hilo, huku wakurugenzi wakitakiwa kuwaondoa maofisa kilimo halmashauri wakafanye kazi kwa wakulima na kuanzisha mashamba darasa ya kufundishia wakulima.

Sisi tunaunga mkono juhudi hizo za serikali za kutaka kuwasaidia wakulima wa zao hilo kwa kuwatafutia soko nje ya nchi, kwani hatua hiyo itasaidia kuwafanya waondokane na hasara zinazotokana na ukosefu wa soko.

Hasara hizo ni pamoja na maparachichi kuoza, kwa sababu ya ukosefu wa soko, kutokana na ukweli kwamba, kuwapo kwa soko la uhakika kunasaidia matunda yasioze na kuuza na kujipatia fedha kwa ajili ya maendeleo yao.

Lakini tunaona ingekuwa vyema zaidi iwapo serikali ingehamasisha pia ujenzi wa viwanda vingi zaidi vya kuchakata matunda nchini, ili wakulima wawe na sehemu badala ya kutegemea vichache vilivyopo. Hatua hiyo inaweza kuongeza soko la ndani kuanzia kwenye maparachichi, machungwa, mananasi na matunda mengine, ambayo yamekuwa yakioza mashambani kutokana na ukosefu wa soko.

Pia kuwapo viwanda vingi vya kuchakata matunda, kutasaidia juhudi za serikali za kutaka Tanzania kuingia katika masoko ya kimataifa kwa kuuza bidhaa zinazotokana na matunda mbalimbali yanayopatikana nchini.

Tunatambua kuwa, lengo la serikali ni kufikia nchi ya viwanda, hivyo nchi ikiwa na viwanda vingi vya kuchakata maparachichi matunda, vitasaidia pia wakulima kuwa na kasi katika kilimo.

Uchache wa viwanda vidogo, kwa namna moja au nyingine, unachangia matunda mbalimbali kuoza mashambani au sokoni na kusababisha hasara kwa wakulima na wafanyabiashara.

Hivyo kwa mtazamo wetu ni kwamba, kuwapo kwa viwanda vingi vya kuchakata matunda nchini, linaweza kuwa suluhisho la hasara ya miaka nenda miaka rudi ambayo wakulima wa matunda wamekuwa wakikumbana nayo.

Tunaamini kwamba mamlaka husika zikiwamo Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zitalichukilia suala hili kwa uzito wake kwa kuwatafutia masoko wakulima wa maparachichi pamoja na kuwahamasisha wawekezaji kuanzisha viwanda vya kuyasindika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge

## Wawekezaji hii ni fursa maeneo ya pembezoni

Na Mary Geofrey

**MWISHONI** mwa mwezi uliopita, Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) imeanza rasmi kutumia mfumo wa kielektroniki (mtandao) kushughulikia maombi ya leseni kubwa na ndogo.

Kwa njia hiyo mwombaji atawasilisha maombi 'online' bila kufika ofisini wala kukutana ana kwa ana na maofisa wa TCRA.

Mfumo huo (License Management System) unazinduliwa na Mawaziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile na Innocent Bashungwa wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambao wizara zao zinasimamia sekta za mawasiliano na utangazaji.

Mkurugenzi wa Leseni na Ufuatiliaji TCRA, John Daffa, akizungumzia mfumo huo mpya anasema ambao ni www.tcra.go.tz utaongeza ufanisi wa upatikanaji leseni kwa wateja wanaonuia kutoa huduma za mawasiliano na utangazaji na kurahisisha mchakato wa kupata huduma kwa muda mfupi.

Lakini, pia utaokoa gharama za ufuatiliaji kwa mwombaji mpya wa leseni au anayetaka kuhuisha leseni yake na utaongeza ufanisi kwa pande zote mbili TCRA na mwombaji, uwazi utaongezeka, utauwezesha mwombaji kupata mrejesho moja kwa moja kwenye simu au email kuhusu hatua zote na maendeleo ya uchakataji wa leseni aliyoomba na kumwezesha mwananchi kuendelea na shughuli za maendeleo badala ya kufuatilia leseni.

Njia hiyo inaelezwa itawezesha muombaji wa leseni ndogo za kuipata ndani ya siku tano wakati kubwa ni siku 45, zamani mteja alikuwa akitumia zaidi ya mwaka kupata leseni kutokana na mfumo uliokuwa unatumika, kwa mujibu wa Daffa.

Anaeleza kuwa, makundi ya leseni yanayopatikana kwenye mfumo huo ambao mwombaji ataweza kuwasilisha maombi yake bila kulazimika kufika katika ofisi za TCRA ni leseni za pamoja zikihusisha leseni za Huduma ya Maudhui (Content Services) na za Mtandao (Network Services).

Leseni nyingine ni Huduma ya Mifumo Tumizi (Application Services), Miundombinu ya Mtandao (Network Facilities), Huduma za Vifurushi na Vipeto, ya Mtumiaji wa Masafa, ya Matengenezo na Usimikaji, Uagizaji Nje na Usambazaji, Rasilimali za Utoaji Namba, ya Huduma za Posta kwa Umma na leseni ya Vifaa Vilivyoidhinishwa.

Anasema hatua ambazo mwombaji wa leseni husika anapaswa kufuata ni pamoja na kutembelea tovuti ya TCRA.

Waziri Ndugulile, akizungumza kabla ya kuzinduliwa kwa mfumo huo anasema, hadi Septemba mosi mwaka huu TCRA itakuwa imekamilisha mapitio yote ili yawasilishwe kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kuanza utelezaji na kwamba tayari wameshafanya maboresho katika suala zima la utoaji wa leseni lakini wanatakiwa kufanya mapitio kwenye tozo na maudhui ya mtandaoni na namna ya kutekeleza lengo ni kuhamasisha uwekezaji mkubwa.

Anaeleza kuwa wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mawasiliano na teknolojia ili kuzifikia wilaya 69 zisizo na redio nchini, na kupitia mfumo huo wanahamasisha wawekezaji kujitokeza ili kufikia wilaya zilizoko pembezoni ambazo hazifikiwi na huduma ya mawasiliano kutokana na sababu za kijiografia.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, anasema mfumo huo utaondoa urasimu kati ya mteja na mtoa huduma kwa sababu maombi yatafanyika mtandaoni na pia utaleta mabadiliko makubwa ya uendeshaji kwa sababu utaongeza weledi na ufanisi kwa wawekezaji kuomba leseni kwa ajili ya uwekezaji kwenye televisheni na redio.

"Mfumo huu unatutoa kwenye mfumo wa zamani wa kuwasiliana kati ya mteja na mtoa huduma uso kwa uso na sasa utaratibu utafanyika kwa sayansi na teknolojia na hata yale mambo mengine ya unanisaidiaje (rushwa) hayatakuwapo," anasema Bashungwa.

# Mahakama yatupa ombi la mawakili utetezi kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imetupilia mbali ombi dogo la mawakili wa upande wa utetezi kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (34) la kutaka maelezo yaliyoandikwa kituo cha polisi na shahidi wa sita wa Jamhuri, Bakari Msangi (38), kusomwa mahakamani kama sehemu ya kumrejeshea kumbukumbu shahidi huyo.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni msaidizi wake wa karibu Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38).

Wakili wa Utetezi, Sylvester Kahunduka, aliwasilisha ombi hilo mahakamani, akidai kwamba shahidi huyo amekuwa akihojiwa mambo mengi na majibu yake yamekuwa hakumbuki au hafahamu.

Alitumia kifungu cha Sheria ya Ushahidi Namba 168 (1,2), kuiomba mahakama hiyo kumsomea maelezo ya awali ya shahidi aliyoandika polisi ili kumrejeshea kumbukumbu.

Naye Fridolin Gwemelo Wakili wa Utetezi pia, aliiomba mahakama apatiwe maelezo ya shahidi ya polisi ili ayatumie kutikisa ushahidi wa shahidi. Shahidi huyo alipewa kielelezo hicho cha nyaraka kuangalia kama anazifahamu na shahidi huyo, alithibitisha kuwa sahihi zilikuwa ni za kwake, lakini alidai kurasa za nyaraka hizo zilikuwa pungufu tofauti na alivyoandika maelezo awali.

Aidha, wakili huyo alidai kuwa pingamizi lililowekwa na Jamhuri la kutaka shahidi kufahamu kama alihojiwa kuhusu kufahamu maelezo yaliyoandikwa kituo cha polisi halikufuata takwa la kisheria.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, alidai kifungu cha sheria ya ushahidi 154 kimeelekeza nini kifanyike kwa kuwa maelezo yanatakiwa yawe yaliondikwa na kuzungumzwa na shahidi na kuwekwa kwenye maandishi.

Alidai kwamba maelezo ya polisi yaliandikishwa bila shahidi kupewa fursa ya kuyapitia na alitakiwa kusaini nyaraka hizo pasipo kufahamu kile kilichoandikwa na askari polisi.

Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, alipinga ombi hilo.

"Utaratibu wa kisheria shahidi lazima atambue maelezo yake aliyoandika kwa utaratibu walipaswa kukumbuka kwa kurejea na maelezo yake aliyoandika kwa kusomewa, kuyaona na kuyatambua."

"Mheshimiwa hakimu ukiangalia upande wa pili wanataka kutumia kifungu hiki cha sheria ya ushahidi kama kumrejeshea kumbukumbu shahidi kwenye maelezo yake ya awali aliyoandika kituo cha polisi, ilhali shahidi huyu, hajaomba kusomewa maelezo hayo kwa ajili ya kurejeshewa kumbukumbu," alidai.

Naye Baraka Mgaya, Wakili wa Serikali, aliomba mahakama hiyo, kumwelekeza wakili wa utetezi kuendelea kumhoji shahidi, badala ya kutumia mlango wa nyuma wa kisheria kutaka shahidi asomewe nyaraka ya polisi ili kumrejeshea kumbukumbu.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, akitoa uamuzi huo mdogo, alisema kifungu cha Sheria ya ushahidi namba 168(1,2), kinapaswa kutumiwa na upande ambao umepeleka shahidi mahakamani na kutupilia mbali ombi la mawakili wa utetezi.

Shahidi huyo, ambaye ni Diwani wa Kata ya Sombetini, jijini Arusha kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), amelitoa ushahidi kwa siku tano mfululizo.

Kesi hiyo imenguruma kwa siku 15 mfululizo katika mahakama hiyo.

Katika hatua nyingine, wakili wa upande wa utetezi, Fridolin Gwemelo, aliwasilisha ombi lingine mahakamani kuomba kutambua maelezo yaliyoandikwa kituo cha polisi kwa kuwa yanatofautiana na ushahidi wake alioutoa mahakamani.

"Hoja yangu huu sio wakati wa kuweka pingamizi au kuonyesha maelezo yamechukuliwa kihalali au hayakuchujwa kihalali bali huu ni wakati wa kumhoji shahidi," alidai.

Akijibu hoja za utetezi, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, alidai kifungu cha Sheria ya ushahidi 154 kimeelekeza nini kifanyike kwa kuwa maelezo yanatakiwa yawe yaliondikwa na kuzungumzwa na shahidi na kuwekwa kwenye maandishi.

"Siyo sahihi kusema wanampitisha shahidi kwenye ushahidi wake wakati alishasema hana ufahamu kwa kile kilichoandikwa ilhali wanatambua na kuelewa kuwa shahidi hafahamu maelezo yaliyoandikwa mbali na kuona sahihi zake na kwa msimamo huu wa sheria vigezo vilivyoainishwa na kifungu cha sheria ya ushahidi namba 154 haiendani na kile kilichotokea."

"Eti wakili anasema tumeweka pingamizi wakati ambao siyo wake na alikuwa anaendelea kujenga hoja, hii sio sahihi kabisa kwa kuwa alianza kwa kumuonyesha shahidi nyaraka ya maelezo kama saini ni za kwake na alikubali, lakini aliieleza mahakama kwamba hafahamu kilichoandikwa ndani kwenye maelezo kwa kuwa hajapata fursa ya kusomewa.

"Si kweli kwamba ni sahihi shahidi akitia saini maelezo yake ikawa ni ya kweli, inawezeka alitia saini lakini maelezo yakawa siyo sawa na sheria haisemi hivyo, pia maswali ambayo alikuwa akiulizwa shahidi yalikuwa yanaendana na maelezo yaliyotolewa polisi."

## Wanaoazimana barakoa waonywa maambukizi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MGANGA Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Isaya Mwasubila, amewatahadharisha wananchi tabia ya kubadilishana barakoa ambayo inadhoofisha mapambano dhidi ya Uviko-19.

Tahadhari hiyo ameitoa juzi wakati akitoa elimu kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Njombe kuwa tayari mjini hamo kuna wagonjwa sita kati yao wawili wamerUhusiwa.

"Kwenye sehemu za kutolea huduma kuna mabango yameandikwa vaa barakoa, kwa hiyo wengine ili aweze kupata huduma anaona bora akachukue barakoa ya mwenzake, wananchi kwenye mikusanyiko wavae barakoa kwa usahihi kwa sababu wasipovaa kwa usahihi mapambano dhidi ya Uviko hayatafanikiwa," alisema.

"Sio tu ilimradi uvae, unakuta mtu hana barakoa anaazima ya mwenzie hii si sahihi ni suala baya sana kwanza linaweza likaongeza kwa kasi kubwa ya maambukizi naomba viongozi, madiwani mnisaidie sana mapambano, siwezi kufanya peke yangu bila nyinyi," alisema Mwasubila.

Aliwataka wafanyabiashara ya kuuza barakoa waache kuwaruhusu wateja kujaribisha kwa kuwa kufanya hivyo ni kusababisha maambukizi.

Kwa upande wake Katibu Tawala, Wilaya ya Njombe, Emmanuel George, alisema maeneo ya kumbi za starehe, harusi na misiba ni sehemu hatari zaidi.

"Kama kwenye misiba, kumbi za starehe, wataalamu wafike kutoa elimu ili kuwanusuru na janga hili," alisema George.

## Kamati kuchunguza chanzo moto kituo cha umeme Moro

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, amesema anaunda kamati ya kuchunguza chanzo cha moto katika kituo cha kupokea na kupooza umeme kilichoko Msamvu, mkoani hapo na kusababisha kukosekana kwa huduma ya umeme katika mkoa huo.

Moto huyo uliolipuka jana asubuhi na kusababisha taharuki kubwa kwa wananchi.

Shigela aliyeambatana na kamati yake ya ulinzi na usalama ya mkoa huo alisema ataunda kamati kwa ajili ya kuchunguza chanzo ili tukio hilo lisijirudie tena.

"Binafsi nimesikitishwa sana na tukio hilo hivyo nachukua fursa hii kuwapa pole TANESCO ikiwa ni pamoja na wananchi wote wa mkoa huu," alisema Shigela.

Alivipongeza vyombo vya ulinzi likiwamo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Mzinga ikiwa ni TANESCO kwa jitihada kubwa za kukabiliana na moto huo. Alisema mbali na kuunda kamati hiyo itakayovihusisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama, pia atahakikisha huduma ya umeme inarudi haraka iwekezanavyo ili wananchi waendelee na shughuli za uzalishaji. Aliwataka wananchi wote wa mkoa huo kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho TANESCO wanashughulikia upatikanaji wa umeme na kuwataka wananchi kuzima vifaa vyao vya umeme kwenye nyumba zao. Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Fragrance Shuma, alisema ajali hiyo ya umeme imesababisha hasara kubwa kwa shirika kwa kuwa kituo hicho kimeungua kwa asilimia kubwa.

Hata hivyo, alisema mitambo yake ni mizima isipokuwa huduma ya umeme haitapatikana kwa urahisi kutokana na mfumo wa udhibiti uliopata tatizo.

"Moto huu umesababisha hitilafu katika kituo hiki hasa kwenye control system (mfumo wa udhibiti), lakini tunafanya jitihada za kupata umeme kutoka Dodoma na Chalinze hivyo huduma itarejea mapema," alisema Fragrance.

Naye Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Fortonatus Muslim, alisema watashirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vya mkoa huo ili kubaini chanzo cha ajali hiyo.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

Responsibilities

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

Qualifications

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

NOTE: This is a commission Based Position

Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.

216387602




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 5 kwa Mkurugenzi wa Ava Group Investment, Judith Karia (kushoto), ambaye ni miongoni mwa washindi kumi wa shindano la benki la ujasiriamali, wakati wa hafla ya makabidhiano Dar es Salaam. Washindi hao kumi walizawadiwa Sh. milioni 5 kila mmoja. **MPIGAPICHA WETU**

# PM aagiza Tanzania na Malawi kuondoa tatizo

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza watendaji wa Mamlaka ya Bandari nchini (TPA), kushirikiana na ubalozi wa Tanzania nchini Malawi kuondoa tatizo la kidiplomasia baina ya mataifa hayo linalosababisha meli zilizojengwa na serikali katika Ziwa Nyasa kuzuiliwa kufanya kazi upande wa Malawi.

Alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kukagua meli ya MV Mbeya Two ambayo ilipata hitilafu mwezi Mei baada ya kupigwa na dhoruba katika eneo la ufukwe wa Matema wakati ikitokea katika Bandari ya Kiwira kwenda Mbamba Bay, mkoani Ruvuma.

Alitoa agizo hilo baada ya Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa TPA, Dk. Baraka Mdima, kumweleza kwamba meli zote tatu za Ziwa Nyasa ambazo mbili ni za mizigo na moja ni ya abiria hazifanyi kazi ya usafirishaji katika upande wa Bandari za Malawi.

Dk. Mdima alisema meli hizo zimekuwa zikizuiliwa na watu wa Malawi wakidai kuwa na wao wanazo za kwao ambazo zinatosheleza mahitaji ya wananchi, lakini uhalisia ni kwamba kuna tatizo la kidiplomasia hasa kwenye shughuli za biashara.

"Tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Malawi ili tutoe huduma na upande wao maana kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukishindwa kuelewana, lakini mpaka sasa tumefikia hatua nzuri na tutaelewana," alisema Dk. Mdima.

Baada ya maelezo hayo, Waziri Mkuu alionyesha kukerwa na ucheleweshaji wa mazungumzo hayo na kuagiza ifikapo Agosti 25, mwaka huu mazungumzo hayo yawe yamekamilika na meli hizo zianze kufanya kazi ili zilete tija zaidi. Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Ismail Mlawa, kuunda uhusiano na ushirikiano na Mkuu wa wilaya jirani ya upande wa Malawi ili vikwazo vya kibiashara visiwe vinatokea.

Alisema katika baadhi ya maeneo nchini wakuu wa wilaya na wakuu wa mikoa ya mipakani, wamejitahidi kutengeneza uhusiano mwema ambao umekuwa na tija kwa taifa akitoa mfano wa uhusiano kati ya Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi pamoja na Jimbo la Tanganyika upande wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera pia kushirikiana na mwenzake wa Malawi kutengeneza ujirani mwema kwa kuwa na vikao vya mara kwa mara ambavyo vitasaidia kuimarisha diplomasia.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliagiza TPA kufanya mazungumzo na wafanyabiashara wa mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na wamiliki wa viwanda wazitumie meli za Ziwa Nyasa kusafirisha bidhaa na malighafi wanazozinunua kutoka nchini Malawi.

Alitoa maagizo hayo baada ya kupata taarifa kwamba meli mbili za mizigo ambazo ni MV Njombe na MV Ruvuma hazijafanya kazi kwa muda mrefu na badala yake zimeegeshwa kwenye Bandari ya Kiwira kutokana na kukosa mizigo ya kusafirisha.

Alisema meli hizo awali zilikuwa zinategemea kusafirisha makaa ya mawe kutoka Liganga na Mchuchuma, lakini baadaye TPA walishindwa kuelewana na mteja wao kuhusu bei na hivyo mteja huyo akaamua kuacha kuzitumia.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi anayeshughulikia Uchukuzi, Mwita Waitara, alisema baada ya meli ya MV Mbeya Two kupata hitilafu alifanya ziara katika bandari hiyo na kubaini kuwa kulikuwa na uzembe wa wasimamizi.

Alisema baada ya kubaini hali hiyo aliamua kumwondoa aliyekuwa Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa pamoja na mmoja wa maofisa wa TPA Makao Makuu na kisha kuwekwa wengine.

Vilevile, aliagiza Kampuni ya Songoro Marine ambayo ndiyo iliyojenga meli hizo kukamilisha ukarabati wa meli ya MV Mbeya Two ili kabla ya Agosti 25 ianze kufanya kazi.

Waziri Mkuu anaendelea na ziara ya siku sita mkoani Mbeya na leo anakusudia kutembelea Wilaya ya Chunya mbako atakagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

# Makinda ahamasisha Watanzania kushiriki sensa

**Na Happy Severine, BARIADI**

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi nchini kwa mwaka 2022, Anna Makinda, amesema ili kuiwezesha serikali kupanga na kufuatilia utekelezaji wa sera na maendeleo ya nchi ni lazima kila Mtanzania ahesabiwe.

Pia amewaomba wananchi kutokusikiliza maneno potofu yanayosemwa kuhusu sensa ya watu na makazi.

Makinda alisema hayo jana wakati wa kujitambulisha kwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David kafulila, ofisini kwake.

Alisema ni lazima kila Mtanzania ashiriki zoezi la kuhesabiwa ili kuisaidia serikali kubaini mahitaji ya msingi ya wananchi wake na wananchi kuacha kusikiliza maneno potofu yanayoongelewa na baadhi ya watu wasio na nia njema. "Sensa ni muhimu kwa maisha yetu na pia kupitia sensa serikali itaweza kupanga na kufuatilia utekelezaji wa maendeleo na mahitaji ya nchi.

Alisema sensa ya mwaka 2022 itakuwa ya kisasa na kipekee zaidi kwa kuwa itaendeshwa kwa mfumo wa TEHAMA ili kuokoa muda na kurahisisha kazi.

Aliongeza kuwa sensa hiyo itahusisha watu wote watakaokuwa wamelala Tanzania usiku wa kuamkia Agosti 8, 2022.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alisema mkoa wake uko tayari kwa sensa hiyo na amewataka wananchi kuwa tayari kupokea kadri ofisi ya takwimu itakavyokuwa imepanga.

# Wakulima kunufaika huduma bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA ambao ni wanachama wa vyama vya ushirika watanufaika kwa huduma ya bima, baada ya mkataba ilioingiwa na taasisi mbili.

Taasisi hizo ni Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ambayo imeingia katika makubaliano na Mfuko wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF), yanayolenga kuwawezesha wakulima walioko ndani ya vyama vya ushirika nchini kuingia kwenye mfumo wa huduma za matibabu kupitia mpango wa bima ya afya kwa wakulima unaojulikana kama Ushirika Afya.

Mpango huo utatekelezwa na benki ya NBC kwa kuwasilisha michango ya Bima ya afya moja kwa moja katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya kwa niaba ya wakulima watakaokuwa na Akaunti Benki ya NBC na kuchukua mikopo ya kilimo kupitia benki hiyo.

Wakizungumza kwenye hafla ya kusaini makubaliano hayo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, walisema mpango huo unalenga kuongeza wigo wa wananchi hususani wakulima katika mfumo wa bima ya afya, hivyo kutekeleza kikamilifu majukumu yao ya kujenga uchumi imara wakiwa na afya njema.

"Sisi kama benki ili tuweze kuendelea kufanya vizuri zaidi tunahitaji kuwa na uchumi imara ambao pia unategemea nguvu kazi yenye afya njema. Suala la huduma afya ya uhakika kwa wateja wetu wakiwamo wakulima na moja ya vipaumbele vyetu na ndio sababu hatukusita kuunga mkono mpango huu wa Ushirika Afya," alisema Sabi.

Kwa mujibu wa Sabi, kupitia mpango huo, mkulima atachangiwa Sh. 76,800 kwa mwaka na ikiwa ana mwenza wake nae atachangiwa kiasi hicho wakati kila mtoto atachangiwa Sh 50,400 kwa mwaka.

"Bima hii itatolewa na NHIF na itapatikana kwenye matawi yote ya NBC nchi nzima, hivyo naomba wakulima wachangamkie fursa hii. Kwa upande wetu maofisa wa benki wamejipanga kuwatembelea wakulima wanachama wa ushirika kuhakikisha wanawapatia habari hii njema kupitia Benki ya NBC," aliongeza Sabi.

Kwa upande wake, Konga aliwahakikishia wakulima wote watakaojiunga na mpango huo kwamba watapata huduma bora kwa urahisi zaidi, huku akibainisha kuwa taasisi hiyo imejipanga kurahisisha huduma kupitia maboresho ya mfumo wake wa TEHAMA.

"Nina imani kupitia ushirikiano wa kihuduma kati ya NBC na wakulima kote nchini mpango huu utakuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa lengo haswa ni kuwafikia wakulima popote walipo ili kuongeza wigo wa wanufaikaji wa mfuko huu," alisema Konga.

HABARI KITAIFA

# TANESCO kuachana na wanaodai rushwa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Nishati, Steven Byabato, ametangaza mwisho wa watumishi wasio waaminifu wanaolichafua Shirika la Umeme (TANESCO) kwa kuwaomba wananchi rushwa ili wawaunganishie umeme.

Amesema hayo jana kwenye ziara ya ukaguzi wa miundombinu ya umeme na kusikiliza matatizo ya wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini kuhusu nishati hiyo akiwa ameambatana na wafanyakazi wa shirika hilo kutoka Makao Makuu, Kanda ya Ziwa na mkoani Kagera.

Byabato alitembelea mitaa mbalimbali katika kata za Nyanga, Buhembe, Kashai na Nshambya, na kusema wakati umefika kwa TANESCO kutoendelea kuchafuliwa na watu wachache, ambao sio waaminifu.

Baada ya kupokea malalamiko ya baadhi ya watumishi kuomba na kupokea rushwa, aliaziga viongozi wa shirika wachukue hatua madhubuti dhidi ya wanajihusisha na uhujumu kwa kupokea rushwa wanapotoa huduma kwa wateja.

# Kilimo cha alizeti chapata mhamasishaji

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI mstaafu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Ruangwa, Nachingwea na Liwale (RUNALI) mkoani Lindi, Hassan Mpako, amesema, baada ya kustaafu, sasa anajikita katika kuhamasisha kilimo cha alizeti.

Mpako ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja kilichopo mjini Liwale, alisema jana kuwa anatamani kilimo cha zao hilo kienee wilayani Liwale kama ilivyo kwenye korosho, ufuta na mbaazi.

"Hiyo ndiyo kazi ambayo ninajipanga kuianza mapema miezi michache ijayo, ili kilimo cha alizeti kiendelee kuenea wilayani mwetu, kwani walikuma wengi bado hajaona umuhimu wa kilimo za zao hilo," alisema Mpako.

Alisema, wakati akiwa kwenye uongozi, alianzisha kilimo cha zao hilo, na kwamba anataka aendelee na kazi ya uhamasishaji ili ikiwezekana, alizeti iwe na umaarufu wilayani, mwake, mkoani Lindi na kusini kwa ujumla.

"Ninakusudia kuanzisha shamba darasa katika mojawapo ya mashamba yangu ya alizeti, ili wakulima waje kujifunza kilimo bora cha alizeti na hatimaye wafaidike na zao hilo," alisema.

Alifafanua kuwa, alipokuwa kwenye uongozi, alipata mafunzo ya kilimo cha alizeti mkoani Dodoma, na kusambaza mafunzo hayo kwa wakulima wenzake, na kwamba anataka apanue zaidi ujuzi huo.

"Tatizo ni kwamba, baadhi ya wakulima, wanaamini kuwa mazao ya biashara ni korosho, ufuta au mbaazi, na kumbe alizeti nayo ina nafasi kubwa ya kuwaingiza fedha, nitaendelea kuhamasisha kilimo cha zao hili," alisema.

# Askofu ataka tahadhari dhidi ya tishio la ugaidi

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

KANISA Katoliki Jimbo la Tunduru- Masasi, limewahimiza wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kuongeza umakini katika ulinzi wa nchi yao hasa kipindi hiki cha tishio la vitendo vya ugaidi.

Hayo yamesemwa na Askofu wa jimbo hilo, Mhashamu Philipo Muhasi, alipokuwa akizungumza na waumizi wa katika Kanisa Kuu la Tunduru, na kuwataka kumcha Mwenyezi Mungu na kuacha tabia za kuuana, kuumizana, kunyonyana, kufanyiana mabaya kwa namna yoyote kwa kuamini kuwa vitu hivyo ni vya kupita.

Askofu Mhasi alisema maelezo hayo anayatoa kufuatia mazungumzo yake na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbbert Ibuge, aliyetembelea ofisini kwake wiki iliyopita, na kwamba, ingawa kwenye mipaka ya Tanzania wapo askari wanaolinda mipaka, lakini wananchi ambao wamekuwa tukipokea wageni kutoka maeneo mbalimbali wanapaswa kuwa makini.

"Ingawa hali ya usalama katika Wilaya ya Tunduru na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla ipo salama, lakini upande wa nchi jirani ya Msumbiji ambayo inapakana na eneo lote la kata zilizopo pembezoni mwa nchi yetu tunapaswa kuwa makini," alisistiza Askofu Muhasi.

Aidha, Askofu Muhasi alieleza kuwa kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa Ibughe, serikali pia imeshatoa maelekezo mbalimbali kwa viongozi wa serikali wakiwamo madiwani, watendaji wa kata na vijiji kuwaelimisha wananchi katika maeneo yao juu ya umuhimu wa kutoa taarifa wanapobaini uwapo wa wageni katika maeneo yao.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, akipongezana na mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mzenga baada ya kupokea meza na viti vilivyotolewa na Benki ya NMB wakati wa hafla iliyofanyika Kisarawe jana. Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali, Vicky Bishubo, Meneja wa NMB tawi la Kisarawe, Justina Kikuli (kushoto). Benki ya NMB kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii (CSR) ilikabidhi madawati na mabati kwa Shule ya Msingi Chanzige A na Sekondari ya Mzenga zote zikiwa wilayani Kisarawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima ufuta wapata bei nzuri

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAKULIMA wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wameuza tani 66,240 za ufuta kwa bei ya Sh. 2,260 kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika mnada wa tisa na wa mwisho uliofanyika katika msimu wa mwaka 2021/2022.

Katika mnada huo ambao ulifanyika viwanja vya Ofisi za Chama cha Ushirika cha Mlingoti Maghalibi Amcos, wanunuzi watatu walijitokeza na kutoa bei mbalimbali ambapo ya chini ilikuwa Sh. 2,000 kwa kila kilo.

Jumla ya Sh. 149,702,4 00 zilipatikana na kuingia kwenye mzunguko wa fedha wilayani humo, baada ya kusambazwa kwa wakulima waliouza ufuta wao kupitia mfumo huo.

Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, Goerge Bisani, alisema kuwa fedha hizo zinatarajiwa kuingizwa kwa wakulima waliokubali kuuza ufuta wao kupitia mfumo huo, baada ya wanunuzi hao kuingiza fedha katika vyama vya ushirka vya wakulima vilivyokusanya ufuta huo.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Imani Kalembo, aliwataka wakulima walioshirki katika mnada huo kuwa makini kusikiliza bei zinazosomwa kutoka kwenye barua za wanunuzi walioomba kununua mazao yao ili kuchagua bei kubwa kuliko zote.

Mwenyekiti wa TAMCU, Mussa Manjaule, pamoja na kumpongeza mnunuzi aliyeshinda tenda ya kununua ufuta huo kwa wakulima, alimtaka kufanya malipo kwa haraka ili kufanikisha malipo ya wakulima kwa wakati.

Alisema Wilaya ya Tunduru imefanya vizuri msimu huo kwa kuuza mazao ya wakulima kwa bei nzuri, na kwamba bado wanaendelea kuwashawishi wakulima ili waendelee kukusanya mazao yao ili waweze kuuza kwa bei ambayo itawawezesha kumudu kurejesha gharama walizotumia na kupata faida.

# DAWASA yatakiwa kuwakatia maji waliounganishwa bomba la hospitali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha (sasa Hanang'), Jenifa Omolo, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kukata maji kwa wateja ambao imewaunganisha kwenye bomba la Hospitali ya Wilaya kwani wanasababisha kukosekana kwa huduma hiyo.

Omolo alitoa ombi hilo juzi wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema halmashauri ilitumia Sh. milioni 21 kwa ajili ya kupeleka bomba kwenye hospitali hiyo, lakini cha kushangaza DAWASA wakaunganisha wateja wao na kusababisha maji kuwa na presha ndogo na wakati mwingine hospitali hiyo kukosa kabisa maji.

"Naomba mkawakatie maji mliowaunganishia kwenye bomba linaloenda hospitali ya wilaya, mnasababisha kero ya maji yanakosekana hospitalini wawekeeni wananchi bomba lao hili liacheni limepelekwa pale kwa fedha za halmashauri, punguzeni hii kero napigiwa simu kila mara maji hakuna," alisema.

Naye Diwani wa Pangani, Augustino Mdachi, alisema kata hiyo inakabiliwa na kero ya maji kwa muda mrefu, lakini shida kubwa ipo katika machinjio iliyojengwa hivi karibuni ambayo haipati maji ya uhakika.

Mdachi alisema halmashauri inalazimika kubeba maji kwa gari kuyapeleka katika machinjio hiyo, jambo ambalo ni gharama nyingine ambazo zinaweza kuepukika endapo DAWASA itapeleka maji kwa haraka.

Diwani wa Picha ya Ndege, Karim Mtambo, alisema kwa sasa Shule ya Sekondari Lulanzi haina maji, hali inayowalazimu wanafunzi kutumia maji ya madimbwi kwa matumizi ya kwenye vyoo.

Mtambo alisema shule hiyo ina matangi ya maji ambayo yanahifadhi maji kipindi cha mvua na kwa sasa wanafunzi wanakabiliwa na kero hiyo kwa kukosa maji ya uhakika kutoka kwenye mabomba.

Diwani wa Tumbi, Raymond Chokala, alisema kata yake ni kati ya maeneo ambayo yana pata maji kwa kusuasua.

Chokala alisema maji katika kata hiyo yanatoka nyakati za usiku kwa kudorora na zipo kaya nyingine ambazo hazipati maji kabisa.

Mhandisi wa miradi DAWASA, Yohana Msangula, alisema atafikisha kero hizo kwa meneja ili zishughulikiwe kwa wakati.

# Kero ya umeme yasababisha mateso zahanati

**Shaban Njia,** KAHAMA

ZAHANATI ya Kijiji cha Ngulu Kata ya Ngogwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, inahudumiwa wagonjwa kwa kutumia tochi za simu za mkononi, kutokana na kukosa umeme tangu kukamilika kwake.

Ujenzi wa zahanati hiyo ulianza tangu Julai 10, mwaka 2008 kwa lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na kuboresha utoaji wa huduma Kata ya Ngogwa na ulianza kutoa huduma kwa wananchi 2,311 tangu Machi mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Noah Bundala, wakati akitoa taarifa ya ujenzi wa zahanati kwa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) Wilaya ya Kahama iliyokuwa ikiongozwa na Katibu na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Emmanuel Mbamange.

Alisema, changamoto inayoikabili zahanati hiyo ni ukosefu wa huduma ya nishati ya umeme, hali ambayo inasababisha kutumia tochi za simu zao za mkononi wakati wa utoaji wa huduma nyakati za usiku hasa inapokea mgonjwa au mjamzito aliyepata tatizo la uzazi.

Pia alisema, ukosefu wa vifaa tiba na vitanda vya kupumzikia na kujifungulia kwa wajawazito unasababisha kuwapeleka wagonjwa katika zahanati jirani ya Ngogwa, na kwamba hata ikipatikana nishati ya jua itasaidia kuondoa tatizo hilo.

Naye mkazi wa kijiji hicho, Sofia Emmanuel, alisema, wamekuwa wakinusurika kuliwa na fisi nyakati za usiku wanaposafirisha wagonjwa au wajawazito kwenda zahanati jirani ya Ngogwa kupata huduma kutokana na zahanati hiyo waliyojengwa kutokuwa na huduma kamili.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kahama, Dk. Lucas David, alisema, kwa mwaka huu wa fedha halmashauri imetenga Sh. milioni 281 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na thamani za ndani katika zahanati tatu za Iponya, Bukooba, Ngulu na Kituo cha Afya Nyashimbi.

Alisema, kati ya fedha hizo, Sh. milioni 100 zitatumika kufunga mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika zahanati hizo na Sh. milioni 181 zitatumika kununua vifaa tiba na dawa.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa CCM Kahama, Emmanuel Mbamange, alisema, kwa hatua ya kwanza umeme umewekwa makao makuu ya kata hiyo, na kwamba baada ya mradi wa umeme vijijini (REA) awamu ya tatu kukamilika umeme utawekwa katika vijiji vyote vya kata ikiwemo zahanati hiyo.

Pia alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama kuhakikisha anafunga umeme wa jua katika zahanati hiyo ili kuendelea kutoa huduma na kuwaondolea adha watoa huduma kutumia tochi za simu wakati wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa.




Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Bank of Africa (BOA), Wasia Mushi, akipatiwa chanjo ya UVIKO-19 katika kituo cha ukumbi wa Mikutano Julius Nyerere jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yasaidia Magereza ujenzi wa zahanati yake

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

BENKI ya Biashara ya Tanzania (TCB) imekabidhi msaada wa mabati 200 kwa Jeshi la Magereza Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa zahanati ya jeshi hilo.

Msaada huo ulikabidhiwa jana mjini Masasi mbele ya Mkuu wa Magereza Wilaya ya Masasi na viongozi wa serikali wa wilaya hiyo akiwamo Mbunge wa Masasi, Geofrey Mwambe.

Akizungumza katika makabidhiano hayo mkurugenzi mkuu wa benki hiyo Tanzania, Sabasaba Mushingi, alisema kuwa benki hiyo imekabidhi msaada huo ukiwa mwendelezo wa kusaidia jamii kama mpango maalum wa sehemu ya faida yake katika jamii.

Mkuu wa Gereza la Wilaya ya Masasi, Modest Magande, aliishukuru benki hiyo ya biashara kwa msaada huo, na kwamba wanatambua mshirikiano wao katika kusaidia jamii.

# Ukonga sasa yaililia TARURA barabara

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Kata ya Ukonga, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam wameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kutenga bajeti kwa ajili ya barabara kutoka eneo la Mombasa kuelekea Moshi Baa, ambayo hairidhishi na kuleta kero kwa watumiaji.

Mmoja wa wakazi wa Mombasa-Ukonga, Alfred Davis, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, alisema pamoja na umuhimu wa barabara hiyo kutokana na kuwapo machinjio ya mifugo ya Mazizini, hakuna kipaumbele katika ujenzi wake.

Alisema machinjio hiyo kila siku huingiza magari makubwa yaliyobeba ng'ombe kutoka mnadani na kufikishwa hapo kwa ajili ya kuchinjwa, serikali ilitakiwa kuimarisha barabara hiyo kiwango cha lami au zege.

"Hii barabara kama ni korofi iwekwe zege kama hata lami ni tatizo. Kwa sababu lami ikiwekwa muda mfupi imebanduka mashimo mengi, bora waichonge si hivi ilivyo sasa," alisema Davis.

Aidha, Maria Mlay ambaye ni mkazi wa Moshi Bar alisema kila siku hutumia barabara hiyo kuelekea Buguruni kununua biashara za chakula kwa jumla, ingawa hofu yake ni barabara hiyo ambayo husababisha baadhi ya magari, bajaji kukataa kubeba abiria na mizigo kuhofia kuharibika kwa vyombo vyao.

"Mfano mimi nauza nyanya, vitunguu yaani genge kwa ujumla, kila alfajiri nipo Buguruni, lakini nikishuka Mombasa ili nielekee Moshi Bar ninakofanyia biashara usafiri huwa mgumu hasa mvua ikinyesha, wenye vyombo vya usafiri wanakataa kutubebea au kupandisha bei ya usafiri, tunaiomba serikali, na viongozi wa huku waichonge hata kama lami haiwezekani," alisema Mariam.

Akizungumza na gazeti hili jana kuhusu suala hilo, Diwani wa Ukonga, Ramadhani Bendera, alisema ameshapeleka maombi ya aidha barabara ichongwe, ijengwe kiwango cha lami, TARURA, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP) na kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Ilala.

Inachotokea ni kwamba Ukonga hatuna chanzo halisi cha mapato ambacho kingesaidia tukarabati mapema barabara hii. Ni tatizo, kero kwa watumiaji nimeliona, na hata alipofanya ziara mbunge wa Jimbo la Ukonga alishuhudia sababu alipita kwa miguu na gari," alisema diwani huyo.

Alisema leo anatarajia kukutana na makandarasi wa kampuni ambayo ni binafsi ili kuzungumza nao namna ya kukarabati barabara kwa kuichonga wakati, wananchi wakisubiria bajeti ya serikali kwa ajili ya ujenzi.

Bendera alisema kifusi kwa ajili ya kufukia mashimo kwenye barabara hiyo ataomba katika kampuni ya ujenzi ya YAPI MERKEZI, ambayo inatekeleza mradi wa reli ya kisasa iliyopo jirani na barabara hiyo.

"Nitatumia mbinu zote ili kufanikisha na hata tutawaomba wafanyabiashara wanaotumia barabara hii na wengine kuchangia fedha hata kwa kuichonga hii barabara, tukisubiri ijengwe."

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 3, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Wazazi wakubaliana kukatwa Sh. 10/- kilo ya ufuta kuchangia ujenzi**



Ukurasa 14

Mbunifu wa VETA anayekomboa wajasiriamali wazalisha sabuni



**Taifa linavyongoja kwa hamu uwekezaji 'huu' wa michezo**

Ukurasa 13

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Unahitajika mjadala wa chakula kitaifa kukabili hofu na usalama

■Ulishaji sumu, kemikali, vyakula feki

WIKI iliyopita Mkutano wa Awali wa Chakula Duniani ulimalizika nchini Italia, ukilenga kuona dunia yenye chakula cha kutosha, kinachozalishwa kwa mifumo salama inayomlinda binadamu, kumpa afya bora pamoja na kulinda mazingira na rasilimali kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Licha ya kwamba dunia inakabiliwa na COVID-19 ni wazi kuwa uwezo wa mwili wa kujikinga na maradhi upo kwenye chakula bora unaoupa kinga na afya kukabiliana na mashambulizi ya magonjwa hivyo siha yaweza kuwa tiba ya magonjwa ya mlipuko.

Hata hivyo wakati mkutano huo umemalizika Julai 28, ni vyema Tanzania nayo ikaandaa mkutano wa kitaifa wa chakula kujadili matatizo yanayokabili sekta hiyo na kuweka mikakati na wahusika wa kuyatatua.

Tatizo la kula mlo kamili na wenye lishe ni kubwa lipo mjini na vijijini na changamoto inayolichochea ni umaskini, elimu duni ya mlo bora, utamaduni na kulishwa 'vyakula umiza'.



Mifugo ikishatibiwa kuna walakini wa kanuni za kuzingatia muda stahiki wa kuuza nyama na maziwa. **PICHA: MTANDAO**

Umaskini unasababisha watu kushindwa kumudu chakula, wakati elimu duni ni tatizo kwa vile watu hawafahamu wanatakiwa muda wote kula mlo kamili wenye wanga, protini, mboga, matunda, madini, mafuta, vitamin, pamoja na maji.

Badala yake hula wanga mwingi pekee kama ugali na mboga kidogo, kipande cha nguru, kachumbari yenye pilipili nyingi.

Utamaduni unatajwa na Ofisa Kilimo Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Margareth Natai, kuwa unachangia ulaji duni, mathalani zipo jamii zinazoamini kuwa chakula ni ndizi pekee au ugali wa mhogo na kisamvu, au makande bila kutumia aina mbalimbali zinazopatikana kwenye maeneo yao.

Anasema utamaduni huo umesababisha baadhi ya jamii kuendeleza ulaji wa mlo wa aina moja kwa miaka mingi na kusababisha udumavu, udhaifu na maradhi yanayohusiana na lishe duni. Hata hivyo, kubwa zama hizi ni kula vyakula vilivyochakachuliwa na kuchafuliwa tena vinavyoumiza.

Mathalani, kwenye masoko mengi ya Dar es Salaam na miji mikubwa ni kawaida mahindi kuchanganywa na mchanga, mawe, magunzi na vumbi linalotokana na kupepeta.

Kuna masoko mtama unajaa mchanga, vipande vya mawe kulingana na rangi yake. Ukiwa mwekundu mchanga mwekundu hutumiwa kadhalika ukiwa mweupe hujazwa taka nyeupe.

Vivyo hivyo kwa choroko na kunde wakati mwingi huchanganywa na mawe na makapi. Kadhalika dagaa nazo zina konokono wadogo na kombe lakini nyingine huchanganywa na nyasi.

Nipashe inapowauliza wafanyabiashara wa nafaka Mbezi jijini Dar es Salaam wanadai kuwa nafaka hufikishwa sokoni zikiwa na taka hizo.

Tofauti na masoko mengine, Soko la Kisutu Dar es Salaam nafaka zimechambuliwa mchele hauna chuya, wala maharage, kunde au karanga huuzwa baada ya kuchambuliwa na bei yake ni kubwa zaidi ikilinganishwa na maeneo mengine.

Kilichobainika ni mazoea ya kuchanganya nafaka na takataka ili kuongeza uzani na kupata faida zaidi ndiyo maana mchele haukosi pumba, chuya na mimea pori inayofanana na mpunga.

Kadhalika, nafaka hizo zinapochambulia mnunuzi huambulia kiasi kidogo kwa vile anatupa uchafu mwingi kutokana na wafanyabiashara kuchakachua bidhaa hizo.

**UCHAKACHUAJI MAZIWA**

Lakini si hivyo tu, maziwa yanayouzwa kwenye migahawa hujazwa maji, au si maziwa halisi, yamechanganywa na ya unga kutoka viwandani.

Maziwa mtindi huchakachuliwa kwa kuchanganywa na unga wa ngano, unaoandaliwa kama uji na kuchanganywa na mtindi ili kuufanya mzito zaidi.

Sababu hizo hupelekea watu kuacha kunywa maziwa mtindi na freshi.

Supu ya pweza na hata kahawa ya alikasusu yapo madai huongezwa vidonge vya kuongeza nguvu za kiume vya viagra. Kadhalika, dawa wanazopewa wanaume na wataalamu wa miti dawa nazo huwekewa vidonge hivyo. Yote hayo yana athari kwa watumiaji.

**KILIO SUMU YA MAFUTA**

Utafiti wa gazeti hili umebaini kuwa wapo watu wanaotumia mafuta kukaanga chips, mihogo, ndizi na hata maandazi kwa miaka mingi.

Hilo hufanyika kwa kuchuja mafuta kwa vitambaa kila yanapochafuka na kuendelea kuyatumia kwa muda mrefu zaidi bila kujali kuwa yanaweza kuwa na athari kubwa kwa walaji kwa vile yamechemka kwa muda mrefu na kwa joto kali na pengine kugeuka sumu.

**MSETO VIBOVU NA VIZIMA**

Wakati mwingine uchafu na uduni wa chakula unadhihirika mtaja anaponunua mfano unga wa dona ulioandaliwa kwa kuchanganya mahindi mabovu na mazima. Mchanganyiko huo husababisha harufu na hata unga kuwa mchungu na watu kushindwa kula.

Aidha, migahawani mchuzi unaandaliwa kwa kutumia nyanya zinazoharibika (masalo) na kuufanya uwe na harufu ya kuchacha.

Kadhalika nyama nazo buchani huchanganywa na zilizoanza kuharibika, matezi na mifupa ili kuongeza uzani lakini pia licha ya wakala wa vipimo kuhakiki kwa kugonga mihuri kwenye mawe ya uzito, wapo baadhi ya wafanyabiashara

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA SABATO KASIKA

## UKOSEFU BWENI

# Wazazi wakubaliana kukatwa Sh. 10/- kilo ya ufuta kuchangia ujenzi



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Maimuna Pathan (wa pili kulia mbele waliokaa), akiwa na viongozi wengine baada ya kumaliza mkutano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKOSEFU wa mabweni kwa baadhi ya shule ni tatizo linalotatiza elimu, kwa kuchochea mimba shuleni, utoro na ufaulu duni lakini pia hukwamisha masomo pale wazazi na walezi wanaposhindwa kuwapangishia watoto wao vyumba jirani na shule.

Katika mazingira hayo, baadhi ya wazazi na walezi wa kata ya Nangano Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, wamekubaliana na uongozi wa kata yao, kujenga mabweni, ili waachane na kupanga vyumba karibu na shule na watoto kushindwa kusoma.

Ni wanavijiji vya Nahoro na Mtungunyu wanaokatwa shilingi 10 kwa kila kilo ya ufuta, kuchangia bweni la Sekondari ya Nangano, kwa mujibu wa Diwani wa Kata hiyo, Abdallah Malombe, anayesema hayo wakati wa mkutano wa wananchi na mbunge wa viti maalum wa Mkoa wa Lindi, Maimuna Pathan, wiki iliyopita.

"Kata hii inaundwa na vijiji vitatu vya Nangano, Nahoro na Matungunyu, ila Nangano ndiko shule ilipo, hivi vingine viko umbali wa kilomita 32, hali ambayo ni tatizo kwa watoto wetu," anasema Malombe.

Anaongeza: " Kutokana na tatizo hilo la umbali, wazazi wamekubali kwa hiari kukatwa Shilingi 10 kwa kila kilo ya ufuta ili kuchangia kujenga bweni la wanafunzi wa kiume."

> "Kata hii inaundwa na vijiji vitatu vya Nangano, Nahoro na Matungunyu, ila Nangano ndiko shule ilipo, hivi vingine...

Katika taarifa yake kwa mbunge Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Nangano Sekondari, Ayubu Mwaigomole, anasema awali shule iligeuza majengo ya maabara kuwa mabweni kwa wanafunzi wavulana.

"Wakati shule inaanza mwaka 2005, wanafunzi wa vijiji hivyo walipangishiwa vyumba na wazazi na walezi lakini walalamika kuwa mazingira si salama kwa maendeleo yao ya elimu," anasema Mwaigomole na kuongeza kuwa baada ya malamamiko hayo, uongozi wa shule ulilazimika kuwahamishia katika majengo ya maabara kwa muda wakati njia nyingine za kuondoa kero hiyo zikitafutwa.

"Tumelazimika kuwaondoa katika majengo hayo, na uhamasishaji ujenzi wa bweni umeanza, kwani taratibu za shule haziruhusu kulaza maabara," anasema na kuonya kuwa baada ya kuwaondoa katika majengo hayo, wanafunzi wamerudi tena kupanga vyumba mitaani, na kwamba wazazi na walezi sasa wanafanya jitihada za kuchanga fedha ili kuunga mkono ujenzi wa bweni.

### OMBI LA MKUU WA SHULE

Mwalimu Mwaigomole anataja mahitaji ya shule mbele ya mbunge huyo kuwa kujenga bweni la wanafunzi 68, jiko la shule na ukarabati wa jengo la utawala, aidha anasema wasichana wana bweni lakini wavulana hasa wanaotoka vijiji vya mbali ndiyo wenye changamoto.

Anasema, wanahitaji kujenga bweni, lakini kuna ukosefu jiko la kupikia chakula cha wanafunzi wakati jengo la utawala linahitaji kukarabatiwa.

"Hayo yote mheshimiwa yanahitaji fedha, hivyo tunakuomba uangalie uwezekano wa kutusaidia chochote utakachoweza ili tufanikishe malengo haya ambayo tumejiwekea," anasema.

Mbali na ombi la mwalimu huyo, mwanafunzi Swadifa Nguate wa kidato cha tatu, alipata nafasi ya kuwawakilisha wenzake na kumweleza mbunge huyo kuwa wanaomba awasaidie kupata taulo za kike za kutosha.

"Mheshimiwa sisi wanafunzi wa kike tuna uhaba wa taulo za kike, hali inayosababisha wakati mwingine tukose vipindi vya masomo darasani anapokuwa katika hedhi, tunaomba utusaidie taulo hizo," anasema Swadifa.

Anafafanua kuwa, baadhi yao hulazimika kukaa katika mabweni wanapokuwa katika hedhi, huku wenzako wakiendelea na vipindi darasani, kutokana na kwamba hawana taulo hizo.

"Tunaomba utusaidie kupata taulo hizo, kwani hata wazazi wetu hawana uwezo wa kumudu gharama zake kwa kila mwezi, hivyo tunakuomba mbunge wetu utusadie kadri Mungu atakavyokujalia," anasema.

### MBUNGE AJIBU MAOMBI

Katika majibu yake, mbunge huyo aliahidi kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wavulana katika shule hiyo, lakini pia kuwanunulia taulo za kike wasichana.

"Kwenye ujenzi wa bweni, nitachangia mifuko 50 ya saruji ili kuongeza nguvu kwenye mikakati yenu, lakini nitamtuma katibu wangu kuangalia ukubwa wa tatizo la taulo za kike," anasema Maimuna.

Anasema, suala la hedhi si la mara moja, bali ni endelevu, kwamba atajitahidi kadri atakavyoweza kuwasaidia wasichana ili kuwa na hedhi salama na kuwawezesha kuhudhuria vipindi vyote vya masomo bila kikwazo.

Mbunge huyo pia anamweleza mwalimu wa kike anayehudumia wanafunzi hao kuwasiliana naye kwa ajili ya majadiliano ya kina ili atakapoanza kusaidia wanafunzi hao awe anajua idadi yao.

Anakiri kuwa, hedhi imekuwa ni kikwazo kwa wanafunzi, kwa kuwa inasababisha baadhi yao kutohudhuria masomo kwa siku kadhaa kwa mwezi, na kwamba wadau wa elimu hawana budi kumaliza kikwazo hicho.

## Unahitajika mjadala wa chakula kitaifa kukabili hofu na usalama

INATOKA UK.11

wanaochezea mizani ili kupima uzito pungufu.

Si chakula pekee hata vinywaji hasa vya kienyeji huchanganywa na dawa za binadamu (antibiotics) kwenye gongo, komoni na mbege.

### KUUA KWA SUMU

Yapo madai kuwa wizi wa nguruwe unatumia kemikali au sumu. Wanyama hao hulishwa sumu kali na wanapolegea wanapasuliwa kuondoa utumbo mara moja na nyama yenye sumu husambazwa kwa walaji mabuchani, baa na nyumbani.

Kemikali hatari zinapotumiwa kulewesha na kuua wanyama kuna uwezekano wa kiasi kingine kuliwa na kudhuru watu hata kuwaua.

Si hivyo tu, hata ng'ombe wanaopewa dawa maziwa yao huuzwa na inapotokea wakizidiwa huchinjwa na nyama kuuza, huku kuku wanaopewa dawa mayai yanauzwa na wakizidwa huuzwa na kuliwa.

Yote hayo yamesababisha watu kula dawa (antibiotic) za wanyama na za binadamu na kusababisha athari ambazo zinahitajika kufanya utafiti na kuzifahamu na kutoa zaidi tahadhari.

Pamoja na wanyama mboga na matunda nayo ni kitisho kwa walaji na hasa zinazozalishwa mijini huongezewa virutisho na viua wadudu bila kuzingatia utaalamu na huuzwa kiholela kwa muda mfupi baada ya kuwekewa dawa, mbolea na busta.

Mboga nyingine humwagiliwa kwa maji machafu yakiwamo yenye taka za vyooni, ya madimbwi sehemu yakaoshewa magari na madumu ya mafuta hasa oili chafu na kuwalisha watu kemikali na vinyesi.

Ndiyo maana Tanzania inahitaji mkutano wa kitaifa wa chakula kuangalia mambo mengi yanayosababisha watu kulishwa vyakula visivyostahili kutumiwa na wanadamu.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Taifa linavyongoja kwa hamu uwekezaji 'huu' wa michezo

SEKTA ya elimu ni muhimu katika kuchagiza kasi ya maendeleo ya nchi na raia wake, ndiyo maana pamoja na jukumu la msingi la taasisi za elimu kuandaa raslimali watu wenye ujuzi, maarifa na stadi stahiki, pia zina wajibu wa kutambua, kukuza na kuendeleza vipaji vya watoto na vijana ili kuzalisha ajira nyingi kuepusha tatizo la ukosefu wa kazi nchini.

Kwa miaka mingi, jamii imeichukulia sekta ya michezo kama eneo la burudani pekee bila kuingalia katika jicho la kukuza na kuendeleza vipaji na ajira, hatimaye serikali kukusanya kodi kwa maendeleo endelevu.

Mitazamo ya kuiona michezo kama jambo la kuburudisha pekee inapaswa kubadilika kwani maendeleo ya sekta hiyo ni chachu ya kukuza vipaji na kutanua wigo wa ajira kwa vijana kwa maendeleo ya taifa.

Mabadiliko ya mtazamo yanastahili kuanza kwa viongozi wa ngazi mbalimbali waliopewa dhamana ya kuongoza nchi na hatimaye yashuke chini hadi kwa wananchi wa kawaida ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu mchango wa michezo katika kuchangia maendeleo ya ukuzaji vipaji na kuongeza fursa za ajira kwa vijana ambao wanakabiliwa na tatizo la kukosa kazi na pia kushindwa kujiajiri.

Juni 8, 2021, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwa mkoani Mtwara katika ufunguzi wa Mashindano ya Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi (UMITASHUMTA) na Sekondari (UMISSETA) anaagiza somo la michezo lifundishwe kwa wanafunzi kote nchini.

"Nasisitiza wizara kuangalia mitaala iliyopo kama inakidhi mahitaji ya sasa na kuchukua hatua stahiki pale ambapo kutaonekana kuna upungufu, nihimize kuboreshwa kwa vyuo vya ualimu na viimarishe masomo ya Elimu kwa Michezo, hatua itakayomwezesha kila mhitimu kuwa na ujuzi wa ufundishaji wa michezo," anasema Waziri Majaliwa.

Hamasa ya wanafunzi kufundishwa somo la michezo ni mwelekeo mzuri wa kufikia lengo la kuwa na wanamichezo walioandaliwa vyema watakaoshiriki kutoa kikamilifu ushindani wa sanaa hasa soka na nyanja nyingine mbalimbali kama muziki, kuogelea na riadha.

Vilevile, akiwa mkoani Mtwara katika ufungaji wa UMISSETA, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, anasema serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha shule maalum za michezo, za msingi na sekondari na vituo maalum vya kuendeleza vipaji vya michezo (sports academies), na kwamba ni kutokana na ukweli kuwa sekta ya michezo ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.

Katika shule hizo, serikali itakuwa mlezi wa kuibua, kulea, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanafunzi ili taifa lijipatie wanamichezo walioandaliwa kikamilifu kimichezo na kitaaluma ili ikiwezekana kuwauza katika soko la ushindani la wanamichezo lililoko duniani sasa.

Wapo wanafunzi wenye vipaji katika michezo ya mpira wa miguu, kikapu, wavu, riadha, kuogelea na ngumi ambao kama watasoma katika shule maalum za michezo wanaweza kufika mbali kimichezo na hivyo kupata ajira katika eneo hilo ambalo kwa sasa wanamichezo wanalipwa fedha pengine kuzidi hata wanaofanya shughuli nyingine za ujasiriamali, kuajiriwa na biashara.

Kutokana na umuhimu wa upatikanaji wa vifaa na mahitaji mengine ya kimichezo, Waziri Bashungwa anaeleza dhamira ya serikali ya kuhakikisha vituo vya michezo vya shule za msingi na serikali vinapatiwa mahitaji muhimu ya kufanikisha azma ya kuendeleza vipaji na michezo.

> "Nasisitiza wizara kuangalia mitaala iliyopo kama inakidhi mahitaji ya sasa na kuchukua hatua stahiki pale ambapo kutaonekana kuna upungufu, nihimize kuboreshwa kwa vyuo vya ualimu na viimarishe masomo ya elimu kwa michezo, hatua itakayomwezesha kila mhitimu kuwa na ujuzi wa ufundishaji wa michezo," anasema Waziri Majaliwa.




Hasheem Thabeet, alipong'ara kwenye Ligi ya mpira wa Kikapu Marekani. Vijana wenye vipaji wakiandaliwa wanaweza kufikia mafanikio makubwa. **PICHA: MTANDAO**

Ni miundombinu kama viwanja vya aina zote, sare, mipira, vifaa, walimu, waamuzi, wote wenye taaluma ya michezo (physical education) ambao ni muhimu kufanikisha mkakati huo ili watoto na vijana watakaopata fursa ya kusoma katika shule hizo wanakuwa wachezaji wenye viwango vya juu na vinavyokidhi ushindani katika soko la ajira la nje na ndani.

Wapo watoto na vijana wengi nchini wenye vipaji katika michezo mbalimbali, lakini wamekosa taasisi imara ya fani hiyo ya kuwaendeleza baadhi yao wamepoteza tumaini la kuja kuwa wasanii na wanamichezo wakubwa kitaifa na kimataifa.

Tanzania ina wanamichezo wa kimataifa kama Simon Msuva anayechezea timu ya Wydad AC wakati nchini Uturuki Mbwana Samatta anacheza kandanda kwenye timu ya Fenerbahce lakini pia alikuwapo Hasheem Thabeet aliyekuwa anacheza kikapu katika Ligi ya Kikapu Marekani (NBA).

Ni vyema mkakati huu wa ujenzi wa shule na vyuo vya michezo ukawekewa msisitizo wa kutosha ikiwamo kutafuta wawekezaji wa ndani na nje ili angalau kuwa na shule moja ya msingi na nyingine ya sekondari ya michezo katika kila wilaya na kuwa na chuo cha michezo katika kila mkoa kutokana na uwepo wa watoto na vijana wengi wanaohitaji kusoma fani hiyo. Wadau wazawa wenye uwezo wa kuwekeza kwenye sekta hiyo waisaidie serikali katika kufanikisha azma hiyo yenye mwelekeo wa kukuza vipaji na kuongeza fursa za ajira kwa vijana na watoto wa taifa hili.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Anapatikana kwa namba: 0620-800462.***

TEKNOLOJIA

NA BEATRICE PHILEMON

# Mbunifu wa VETA anayekomboa wajasiriamali wazalisha sabuni




Fundi Ramadhan Muzii, akielezea wateja jinsi mashine ya kutengeneza sabuni ya vipande inavyofanya kazi katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba hivi karibuni. **PICHA : BEATRICE PHILEMON.**

BAADA ya kuhitimu kozi ya ufundi akisomea 'fitter mechanics', katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) Morogoro, Ramadhan Muzii, anakuwa mkombozi wa wajasiriamali wanaozalisha sabuni za mche.

Alipomaliza masomo kwa miaka mitatu amekuja na jibu la kuwapunguzia mzigo kinamama wazalishaji bidhaa hiyo wa mikoa mbalimbali, anasema wanatumia muda mwingi na nguvu nyingi kuchanganya viambato vya kutengeneza sabuni na kuchosha mwili na mikono.

Mtaalamu huyo anataja baadhi ya viambato vinavyotumiwa kuwa ni pamoja na mafuta ya mawese, mise inayotoka ndani ya chikichiki na tindikali ya 'caustic soda.'

Muzii, amegundua mashine ya kutengeneza sabuni inayofanya kazi kwa wepesi na kwa tija yenye uwezo wa kuzalisha miche 1,000 kwa siku, wakati kwa kipindi mjasiriamali anatengeneza miche 100 mpaka 200.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, anasema mashine hiyo ameipa jina la 'bar soap making machine,' inatumia umeme wa njia tatu (three phase) na gharama yake ni milioni 14.

Muzii, aliyesoma ufundi wa mitambo, anawashauri wajasiriamali wanaopenda kuanzisha viwanda vidogo vya kuzalisha sababu za miche kuungana kununua mitambo ili kuchanganya na kutengeneza bidhaa hizo zinazohitaji kila wakati.

Anaongeza kuwa mbali na hilo, kampuni yao inatengeneza mashine hizo kulingana na mahitaji ya mteja.

> "Tunaomba msaada kwa sababu baadhi ya vifaa vya kufundishia vimeanza kuchakaa na wanafunzi wakihitaji kufanya mazoezi inabidi twende kuazima kwa watu binafsi," anasema.

"Mjasiriamali akinunua mashine yetu tunamsafirishia bure kwenda kwake na pia kumpa mafunzo ya kuitumia," anasema Mzee.

Mtaalamu huyo ambaye ni fundi mkuu katika kampuni ya JPW Robot Machinery ya Dar es Salaam anasema maeneo mengi nchini kinamama wajasiriamali wanachangamoto kubwa kwa sababu wanatumia maboksi ya mbao kutengeneza sabuni na kusababisha sabuni kuwa na maumbo mabaya licha ya kutumia nguvu nyingi.

Anasema wametengeneza zaidi ya mashine 10 zilizouzwa Comoro na Zambia. Lakini nyingine zimenunuliwa na wateja wa Geita, Singida, Dar es Salaam na wanaendelea kuzalisha kwa watu mbalimbali waliomba.

"Kwa sasa wajasiriamali wanaweza kupata mashine hizi hapa nchini badala ya kuziagiza China na nchi nyingine za Asia," anasema Muzii.

### SOKO LA MASHINE

Anasema ingawa kuna mafundi wengi (technicians) waliosoma nje na vyuo vya VETA ambao wametengeneza mashine za aina mbalimbali zenye ubora wa hali ya juu, bado nyingi hazijulikani.

"Kutokana na changamoto hii, tunaiomba serikali iwathamini vijana wanaounda mashine tofauti na kuwapa mitaji, kuwatafutia masoko ya mashine nje na ndani pia kuwasaidia kutatua changamoto zao hasa upatikanaji wa vifaa vya kuviunda mashine kwa sababu mafundi wengi wapo mitaani na hawana msimamizi," anasema Muzii.

Mbali na hilo mafundi wanaiomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, ifanye utafiti nchi nzima ili kujua Tanzania ina mafundi mchundo (technicians) wangapi ambao wapo mitaani, aina za mashine wanazozalisha, changamoto walizonazo, wanachohitaji kutoka serikalini ili waweze kufanya kazi katika mazingira bora, lakini taifa liwe takwimu sahihi za mafundi.

Nchi ina aina mbalimbali za mashine zenye ubora wa hali ya juu lakini hazijulikani kitu ambacho kinachangia wajasiriamali wengine kuziagiza nje, anasema.

Kutokana na changamoto hiyo, wizara inatakiwa isimamie eneo hilo ili wajulikane na kuuza bidhaa zao kwa urahisi kwa sababu mafundi wengi wana bidhaa nzuri zilizoko mitaani lakini hazijulikani.

Utafiti huo utasaidia serikali kuwa na takwimu sahihi kuhusu mafundi, kutatua changamoto zao kwa urahisi, mafundi na wabunifu (innovators) kutoa huduma inayotakiwa kwa wateja wao.

"Watu wengi wanahitaji mashine tofauti tofauti lakini wanashindwa kuzipata Tanzania kwa sababu mafundi wengi wapo mitaani hawana usimamizi kitu kinachochangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kupata soko la bidhaa zao.

### WITO KWA SERIKALI

"Tunaomba serikali itusimamie katika upatikanaji wa vifaa vya kutengeneza mashine za aina mbalimbali kwa sababu, wengi wanaagiza vifaa nje lakini kila mtu anajitegemea," anasema Muzii.

Anasema lakini, serikali ingekuwa inasimamia suala hilo wangekuwa wanapata wateja mbalimbali wanunuzi, na kupata urahisi wa kuagiza vifaa nje ya nchi na kupata kirahisi kuliko mtu binafsi.

Anasema mjasiriamali mdogo inakuwa ngumu kuagiza vifaa, "Tunaomba serikali itusimamie katika uingizaji wa vifaa kutoka nje ya nchi kama vile electric motors, gear boxes na vingine kutoka China.

### HISTORIA YAKE

Anawashauri vijana wajitume kufanya kazi, fursa zipo nyingi kwa mfano kuunda mashine na kilimo ambavyo vinaweza kuwainua na kujipatia kipato na ajira.

Muzii amezaliwa Kidogobasi, Wilaya ya Kilombero mkoa wa Morogoro, alianza kutengeneza mashine mwaka 2019 baada ya kupata mafunzo ya ufundi katika Chuo cha VETA-Morogoro.

"Niliamua kutengeneza mashine hii ili kujipatia kipato na kuendeleza maisha yangu kwa sababu nimesoma ufundi kwa hiyo naendeleza maisha yangu kupitia ufundi."

Naamini mashine hii itawarahisishia kazi kinamama na wengine kwenye shughuli za uchanganyaji na utengenezaji wa sabuni.

Mwalimu wa Ufundi wa VETA-Morogoro, Fredrick Notley, anawaomba wadau kuwapa fedha ili wanunue vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufundishia na kutengeneza mashine kwa wingi na kuziingiza sokoni.

"Tunaomba msaada kwa sababu baadhi ya vifaa vya kufundishia vimeanza kuchakaa na wanafunzi wakihitaji kufanya mazoezi inabidi twende kuazima kwa watu binafsi," anasema.

Wanahitaji mashine ya kuunga vyuma, kukata, kukunja, kusokotea mabati, nyingine ni ya kutobolea na kukereza vyuma na ya kukatulia vyuma vyote vikiwa na thamani ya Shilingi milioni 350.

Anasema vifaa hivi vikipatikana vitafundishia wanafunzi na kuzalisha bidhaa kwa wingi.

Mbali na hilo, kwa upande wa mfumo wa umeme, bado wanahitaji PCB Printing Machine ambayo thamani yake ni shilingi milioni 20.

Meneja Uhusiano VETA - Dar es Salaam, Sitta Peter, anasema VETA itaendelea kuboresha maeneo yote yenye vyuo vyake ambavyo vina changamoto ili kusaidia wanafunzi kusoma katika mazingira wezeshi kuzalisha mafundi wenye ujuzi wa kutosha, lakini kuwasaidia kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Anasema kwa kuanza tayari wameboresha vyuo vya Arusha, Kihonda -Morogoro na VETA Mwanza.



## HABARI DODOMA

## Wajasiriamali waandaa maonyesho ya bidhaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya serikali kufuta Maonyesho ya Wakulima Nanenane mwaka huu, umoja wa wajasiriamali Kwanza umeandaa maonyesho ya bidhaa mbalimbali yatakayofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa umoja huo, Haruna Kifimbo, alisema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maonyesho hayo.

Kifimbo alisema maonyesho hayo yanatarajiwa kushirikisha zaidi ya wajasiriamali 700, ambao wataleta na kuonyesha bidhaa zao mbalimbali kutoka maeneo yote nchini.

"Kutokana na serikali kufuta maonyesho ya Nanenae mwaka huu sisi kama wajasiriamali tumeona siku hizi zisipite bure, hivyo tumeandaa maonyesho haya ambayo yatahusisha watu mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali ya nchi," alisema Kifimbo.

Aidha, alisema kuwa maonyesho hayo yatafanyika kuanzia Agosti 1, hadi 13, ambapo pamoja na wajasiriamali makundi mengine kama Wizara ya Maliasili na Utalii watakuwapo pia kuonyesha shughuli zao.

Kadhalika, Kifimbo alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wajasiriamali nchini wakiwamo wa Jiji la Dodoma kutangaza bidhaa wanazozalisha na kuongeza wigo wa masoko.

Vilevile, alisema kuwa mkoa tayari umeshawapatia barua ya kuruhusu wao kufanya maonyesho hayo ya wajasiriamali katika muda huo.

Mapema mwaka huu Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ilitanga kufuta maonyesho ya Nanenae.

Waziri Mkenda alisema sababu kubwa ni kuitumia fedha ambazo zingetumika katika maonyesho hayo ili kuimarisha shughuli za ugani na kuongeza tija kwenye kilimo.

**"Kutokana na serikali kufuta maonyesho ya Nanenae mwaka huu sisi kama wajasiriamali tumeona siku hizi zisipite bure, hivyo tumeandaa maonyesho haya ambayo yatahusisha watu mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali ya nchi," alisema Kifimbo.**

# Viongozi wa dini waombwa kuhamasisha chanjo corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amewaomba viongozi wa dini nchini kuhamasisha waumini wao kushiriki upataji wa chanjo inayotolewa bure na serikali ili kujilinda dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa Uviko-19.

Mtaka alitoa ushauri huo juzi jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na viongozi wa Kanisala Aglikana Tanzania Dayosisi ya Kati kwenye mkutano wa Sinodi ya 21.

Alisema viongozi wa dini hawanabudi kuwaelimisha waumini wao ili waweze kupata chanjo hiyo inayotolewa hivi sasa kwa makundi mbalimbali ya watu.

"Katika suala hili tuache kabisa siasa kwani afya ni mali yako wewe siyo ya serikali, utakufa na serikali utaiacha hivyo tuitumie fursa hii ya chanjo inayotolewa bure na serikali ili kuchanja na kujilinda dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona," alisema Mtaka.

Alisema maneno ambayo yamekuwa yakienezwa katika mitandao ya kijamii juu ya ubora wa hiyo chanjo yanatakiwa kupuuzwa.

"Huko kwenye mitandao ndiko watu wanapotoshana unaweza kuta mtu anasema chanjo haifai unabishana naye kumbe mwenzio tayari alishachanja, hivyo viongozi wa dini mnatakiwa kulikemea hili kwani mambo ya chanjo hayajaanza leo yapo toka zama hizo," alisema Mtaka. Kadhalika, aliwataka wakazi wa mkoa wa Dodoma kujitokeza kwa wingi chanjo itakapoanza kutolewa katika vituo mbalimbali vilivyopangwa.

"Mpaka hivi sasa kuna watu zaidi ya 1,000 ambao wamenipigia simu wanataka kuja kuchanja chanjo hii itakapoanza kutolewa na wataalamu wa afya mkoani kwetu," alisema Mtaka.

Aidha, alisema chanjo hiyo kwa mujibu wa watalaamu wa afya ni salama, hivyo kila Mtanzania kwa hiyari yake anao wajibu wa kushiriki ili kupunguza hatari za ugonjwa wa corona wimbi la tatu.

Vilevile, Mtaka aliwaomba viongozi hao kuhamasisha waumini wao kujiunga na mifuko ya bima ya afya ili wapate matibabu ya uhakika na wakati wote.

"Watu wakijiunga na mifuko hii ya bima ya afya itasaidia kuondoa kero ambazo zimekuwa zikijitokeza hasa wakati wanapougua," alisema Mtaka.




Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya (kulia), akimkabidhi cheti Naomi Mmanyi mwanafunzi wa Chuo cha Ushonaji cha Young Women's Christian Association (YWCA) tawi la Dodoma kwenye mahafali ya 83 iliyofanyika juzi jijini Dodoma. **PICHA: INRAHIM JOSEPH**

# Mfumo wasajili wakulima wa mikoa 14

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ZAIDI ya mikoa 14 nchini imefanikiwa kusajili wakulima kwenye mfumo wa M-Kilimo unaoendeshwa chini ya wizara ya kilimo ili kuwarahishia kupata huduma za ugani kutoka serikalini.

Pia, wizara hiyo kwa kushirikiana na TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Serikali za Mitaa bado zinaendelea na usajili wa wakulima kwenye mfumo wa M-Kilimo ili waweze kutambuliwa.

Akizungumzia usajili wa wakulima Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, alisema kuwa mikoa 12 bado ipo chini ya asilimia 50 kwenye usajili wa wakulima.

Prof. Tumbo alieleza kuwa mikoa minne ambayo ni Njombe, Arusha, Simiyu na Singida imefikia lengo la asilimia 100 na zaidi na kuipongeza huku akitaka mikoa mingine kuiga mfano huo.

"Wizara ya Kilimo inaipongeza sana mikoa hii kwa kufikia hatua hiyo naomba na mikoa mingine muige mfano lengo ni kuona wakulima mnapata huduma za kiugani baada ya kusajiliwa ili kufanya kilimo chenye tija," alisema Prof. Tumbo.

Alisema kuwa Mikoa ya Shinyanga, Kagera na Dar-es-Salaam bado wapo chini ya asilimia 30, hivyo ameitaka kuongeza kasi ya usajili ili kufikia malengo ya serikali.

"Pia Wizara ya Kilimo inatoa pongezi kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, watendaji wakuu na wakati katika ngazi ya mikoa na wilaya, halmashauri na maofisa kilimo na wagani wote kwa kazi kubwa ya kuwezesha, kuhamasisha na kusajili wakulima kwenye mfumo wa M-Kilimo," alisema.

Wizara ya Kilimo ilizindua mfumo wa M-Kilimo kwa lengo la kuwatambua wakulima wake ikiwamo kuwasaidia kupata huduma za kiugani ili wafanye kilimo chenye tija ambacho kitawapa manufaa wao na taifa kwa ujumla.



# Majaliwa apiga marufuku lumbesa viazi mviringo

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amepiga marufuku wafanyabiashara kununua mazao ya wakulima kwa kutumia vipimo visivyokuwa rasmi ikiwamo kutumia lumbesa akidai kuwa vipimo hivyo vinatumika kuwaibia wakulima.

Alipiga marufuku hiyo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi wa Wilaya ya Rungwe katika Kijiji cha Ilolo Kata ya Kiwira, ambapo alisema msimamo wa serikali ni kuhakikisha mfumo wa lumbesa kwenye biashara ya mazao unakomeshwa.

Alisema matumizi ya lumbesa yamekuwa yakiwaumiza zaidi wakulima wa viazi mviringo ambavyo ni miongoni mwa mazao yanayozalishwa kwa wingi katika mikoa ya Mbeya na Njombe.

Waziri Mkuu alisema kipimo kinachokubalika kwenye biashara ya mazao ni mizani na kwamba gunia lolote linalotumika ni lenye uzito wa kilo 100 na sio zaidi ya hapo na kwamba ukitumika mfumo mwingine ni wizi.

"Mtu ananunua gunia la viazi lenye ujazo wa kilo 100 halafu anaongezea kipeto kingine juu cha kilo 20 ambazo hazilipi, huo ni wizi na namwagiza Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aondoe vipimo vya aina hiyo sokoni ili wakulima wanufaike na jasho lao," alisema Majaliwa.

Aliagiza Wizara ya Kilimo kusimamia matumizi ya mizani kwenye maeneo ya masoko hasa maeneo ya vijijini ili kukomesha matumizi ya vipimo visivyokuwa rasmi ikiwa ni pamoja na matumizi ya ndoo za lita 20 na vipimo vingine.

Bashe alisema hivi karibuni anakusudia kuitisha kikao maalum na wakuu wa mikoa yote inayozalisha viazi mviringo ili kujadiliana na kuweka mikakati ya kukomesha lumbesa.

Alisema wakulima wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwenye uzalishaji wa mazao yao, lakini hawanufaiki nayo kutokana na uhuni unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wanaowarubuni kwa kutumia vipimo visivyo halali.

"Hiki kilio cha lumbesa ni cha muda mrefu na wakulima wameumia sana, sasa sisi kama serikali ni lazima tuje na suluhisho, kwenye kikao hicho na wakuu wa mikoa pia tutawashirikisha wadau wengine ili tuwe na sauti moja," alisema Bashe.

Vilevile alisema wizara yake itaendelea kusimamia mazao mengine yakiwamo yale ya kipaumbele ikiwamo korosho, chai, kahawa, chikichi na mazao mengine muhimu ili kuhakikisha yanasaidia.

Awali Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Anthon Mwantono, alisema Wilaya ya Rungwe ni miongoni mwa wilaya zinazozalisha viazi kwa wingi, lakini tatizo kubwa linalowakatisha tamaa wakulima ni bei kuwa chini pamoja na vipimo visivyoruhusiwa.

Alisema pembejeo zinauzwa kwa bei ya juu kuliko kile ambacho wakulima wanapata baada ya kuuza mazao yao, hivyo akaiomba Serikali kuwasaidia wakulima kukabiliana na tatizo hilo ambalo alidai limekuwa sugu.

Alisema wakati mwingine wakulima wanalazimika kuuza mazao yao kwa lumbesa kutokana na kutokuwa na uhakika wa kupata soko linguine endapo wanunuzi wanaotaka kununua kwa lumbesa wataacha kununua mazao yao.

Naye Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Sophia Mwakagenda, alisema tatizo hilo linaweza likakomeshwa kama ambavyo Waziri Mkuu alitumia mbinu kutatua migogoro ya bei ya chai wilayani humo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akimpa maelekezo Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa (katikati), kuanza vikao vya ujirani mwema na wilaya za nchi ya Malawi ambazo zinapakana na Ziwa Nyasa ili kutengeneza fursa za uwekezaji kupitia usafiri wa meli katika Bandari ya Itunge, (kulia) ni Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mwita Waitara, kwenye ziara wilayani Kyela. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wahadhiri fani ufugaji nyuki wasakwa SUA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MENEJIMENTI ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) kimeanza mikakati ya kutafuta wahadhiri kutoka nje ya chuo hicho kwa ajili ya kufundisha fani mpya ya ufugaji nyuki katika Ndaki ya Mizengo Pinda iliyoko mkoani Katavi ili kuzalisha wataalamu wa fani hiyo nchini.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. George Mwamengele, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wajumbe wa Bodi ya Chuo hicho walipofanya ziara ya kukagua miradi ya chuo hicho ambapo alisema fani hiyo haina wataalamu kutokana na kuwa mpya chuoni hapo.

Alisema kabla ndaki hiyo haijaanzishwa Kampasi Kuu ya Chuo hicho iliyopo mkoani Morogoro haikuwa na fani hiyo kabisa na hivyo kusababisha ugumu wa upatikanaji wa wataalamu baada ya fani hiyo kuanzishwa.

Alisema wanatarajia kuwapata wakufunzi wa fani hiyo kutoka katika vyuo vingine vikiwamo vya nje ya nchi ili kuhakikisha fani hiyo inapata wataalamu na kuifanya sekta ya ufugaji wa nyuki kuwa moja ya vyanzo vya mapato ya serikali.

"Kuna baadhi ya masomo tumeanzisha hapa ambayo kule 'Main Campus' (Kampasi kuu) hatukuwa nayo, hii shahada ya nyuki na mazao ya nyuki ni mpya kabisa, kwa hiyo hii fani pamoja na zingine hatuna walimu," alisema Prof. Mwamengele.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Anna Sikira, aliwataka vijana wa Tanzania na nje ya Tanzania kuchangamkia kujiunga na fani zinazofundishwa chuoni hapo kutokana na kuwa na uhakika wa kuajiriwa ama kujiajiri.

Aliwataka vijana kuchangamkia fani ya nyuki na mazao yake kutokana na kuwa mpya na yenye fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kuwa miongoni mwa fani zinazozingatia zaidi ubunifu.

"Hiki ndio chuo pekee nchini ambacho kinatoa digrii ya ufugaji nyuki pamoja na mazao ya nyuki, kwahiyo nawashauri vijana wachangamke kuja kusoma hapa ili wawe na uhakika wa ajira, hapa mtu anapata ujuzi ambao utamuwezesha hata kujiajiri yeye mwenyewe," alisema Prof. Sikira.

Alisema mbali na fani hiyo ya ufugaji nyuki pia ndaki hiyo inafundisha fani ya kilimo ambayo ni miongoni mwa fani zenye fursa nyingi nchini na nje ya nchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Ndaki hiyo, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema katika kipindi chake cha uongozi atahakikisha ndaki hiyo inazalisha wataalamu wa kutosha katika fani tofauti kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema wanategemea kuifanya ndaki hiyo ya Mizengo Pinda kuwa miongoni mwa taasisi zinazotegemewa na wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na taifa kutokana na kuzalisha wataalamu wengi.

Alisema wataalamu wanaozalishwa katika ndaki hiyo watasaidia taifa kutatua matatizo ambayo yanazikabili sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, utalii, viwanda na sekta zingine na kuziwezesha sekta hizo kuchangia pato la taifa.

"Ndaki hii inafundisha mambo ambayo wananchi wanashughulika nayo kila siku, kwa hiyo hawa vijana wanaozalishwa hapa kazi yao kubwa ni kuhakikisha wanawasaidia wananchi kuboresha mambo haya kwa kutumia utaalamu ambao wataupata," alisema Dk. Bucheyeki.

# Wakulima waiomba serikali soko la pareto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa pareto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kutafuta wanunuzi wengine wa zao hilo ili kuongeza ushindani utakaosababisha bei ya zao hilo kupanda na kuwanufaisha.

Wakulima hao wa vijiji mbalimbali vya eneo la Umalila wilayani humo walitoa ombi hilo juzi walipokuwa wanapokea vifaa mbalimbali vya ujenzi wa miundombinu ya shule, afya na barabara kwenye maeneo yao.

Vifaa hivyo vilitolewa na kampuni inayonunua zao hilo katika wilaya hiyo ijulikanayo kwa jina la Pyrethrum Company of Tanzania (PCT) ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa kampuni hiyo kushiriki kwenye shughuli za kijamii kwenye maeneo ambayo inanunua zao hilo.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Joseph Mwile, alisema awali walikuwa wanauza zao hilo kwa bei kati ya Sh. 2,400 na 2,500 kwa kilo moja lakini kwa sasa imepanda na kufikia Sh. 2,700 bei ambayo alidai bado haina tija kwao.Alisema angalau bei ya zao hilo ingepanda na kufikia Sh. 3,000 kwa kilo akidai kuwa kazi ya kuzalisha zao hilo ni ngumu na inawachukua muda mrefu mpaka kufikia hatua ya kuuza.

"Mimi nina ekari tano, siwezi kuzihudumia peke yangu lazima niweke vibarua wa kunisaidia, lakini kwa bei tunazouza pareto hii kwa sasa huwezi ukapata faida, tunaomba angalau serikali itusaidie kupata wanunuzi wengine," alisema Mwile.

Naye Iyela Mwaweza ambaye ni mkulima wa Kijiji cha Pashungu alisema wakazi wengi wa kijiji hicho wanalima pareto lakini kutokana na mnunuzi kuwa mmoja fedha huwa zinaisha kwa mawakala na kusababisha baadhi yao kushindwa kuuza.

Alisema wakulima wanapoamua kuuza mazao yao wanakuwa wamejiwekea malengo yao hivyo kitendo cha kukosa fedha kwa mawakala kinawasababishia kukwama kutekeleza malengo yao, hivyo akaomba tatizo hilo litatuliwe.

"Wakati mwingine unaenda kuuza pareto yako unakuta ofisi imefungwa, ukiuliza unaambiwa fedha hamna na huwezi kuuza kwingine mnunuzi ni huyohuyo mmoja, hii ni kero kubwa kwetu," alisema Mwaweza.

Wawakilishi wa Kampuni ya PCT waliahidi kutatua kero ambazo zipo ndani ya uwezo wao huku wakiwaomba wadau wengine kusaidia kwenye utatuzi wa matatizo yanayowakabili wakulima hao ili kilimo cha pareto kiendelee kukua.





# Rais Mwinyi awaapisha Makatibu Wakuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaapisha Makatibu Wakuu mbalimbali aliowateua Julai 30, 2021, kushika nyadhifa hizo.

Katika hafla hiyo iliyofanyika Ikulu jijini Zanzibar, Dk. Mwinyi amemwapisha Dk. Omar Dadi Shajak, kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar pamoja na Khadija Khamis Rajab, kuwa Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya Kazi na Uwezeshaji katika Wizara ya Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Pia amemwapisha Dk. Habiba Hassan Omar, kuwa Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya uchumi na uwekezaji katika Wizara ya Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Dk. Fatma Haji Khafidh kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto.

Wengine walioapishwa ni Khamis Kona Khamis, (aliemteua Julai 16, 2021) kushika wadhifa wa Mkurugenzi Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Kwa upande wao baadhi ya watendaji walioapishwa, walisema watashirikiana na watendaji pamoja na wadau mbalimbali katika maeneo yao ili kuhakikisha wanafikia malengo.

"Nitatumia nguvu na uwezo wangu wote kushirikiana na watendaji wa Tume na wadau mbalimbali wa uchaguzi kufanikisha masuala ya msingi ya Tume hiyo," alisema Mkurugenzi Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Khamis Kona Khamis.

Alisema majukumu ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kimsingi yameanishwa kisheria, atajitahidi kusogeza mbele majukumu hayo ili kufikia malengo.

Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya uchumi na Uwekezaji katika Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema ataimarisha uwekezaji na kuhakikisha anapunguza changamoto mbalimbali ziliopo ikiwamo urasimu, huku akiunga mkono hatua ya Mamalaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), kuanzisha 'One Stop centre', pamoja na kuainisha umuhimu wa kuendeleza uwekezaji kwa njia ya ubia (Public Private Partnership - PPP).

Viongozi mbalimbali walishiriki katika hafla hiyo, akiwamo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji na Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi Idrissa Kitwana Mustafa.

# Watakiwa kutumia fursa ya mtandao kujifunza

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WATAALAMU mbalimbali wa masuala ya elimu wameeleza nafasi ya mtandao wa 4G katika kuendeleza sekta ya elimu ikiwamo walimu na wanafunzi kutumia fursa hiyo kama nyenzo muhimu ya kufundishia na kujifunzia ili kuendana na kasi ya ulimwengu wa kidigitali.

Hayo yalibainishwa jana katika warsha maalumu iliyoandaliwa na Kampuni ya Mawasiliano ya Zantel kujadili umuhimu wa mtandao wa 4G katika kuboresha elimu visiwani humo ambayo ilihudhuriwa na wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali, mjini Vuga.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa warsha hiyo, Meneja Chapa wa Zantel kwa niaba ya Mkuu wa Zantel-Zanzibar, David Maisori, alisema warsha hiyo ililenga kujadili kiundani namna gani wadau wa elimu wanavyoweza kutumia intaneti kuendeleza na kuboresha utendaji kazi katika sekta hiyo.

"Kampuni yetu ya Zantel imefanya kazi kubwa sana ya kujenga miundombinu ya mtandao wenye kasi wa 4G hapa Zanzibar. Tuna minara zaidi ya 100 inayotoa huduma ya mtandao wa 4G kote Unguja na Pemba hivyo kazi ni kwenu sasa wanafunzi, walimu na wahadhili, serikali, taasisi na wadau wengine wa elimu kutumia miundombinu iliyopo ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia," alisema.

Alisema wanafunzi wana uwanja mpana zaidi wa kuendeleza taaluma zao na kupitia mtandao wanaweza kufanya mambo mengi zaidi ya kuwanufaisha kielimu mbali na kutumia katika mitandao ya kijamii pekee.

Naye Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Omari Saidi Ali, alisema serikali imefanya juhudi kubwa kuboresha miundombinu ikiwamo kujenga mkongo wa taifa mawasiliano na minara ya mawasiliano ili kuhakikisha huduma zinakuwa za uhakika na nafuu.

"Tumefanya jitihada hizi ili nchi yetu iendane na karne ya maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na kuanzisha tume mbalimbali za usimamizi. Lakini tumeweka sera ikiwamo sera ya serikali mtandao ili kuchochea matumizi ya mtandao," alisema.

Alitoa mfano kipindi hiki ambacho dunia imekumbwa na ugonjwa wa virusi vya corona, mtandao umegeuka kuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano hasa kwa kufundishia kutokana na shule kufungwa na kufanya intaneti kuwa mkombozi mkubwa katika kuendeleza elimu.

Aliipongeza Zantel kwa jitihada za kuhakikisha mtandao wa 4G unawafikia watu wengi zaidi pamoja na unafuu wa huduma zake ikiwamo kwa wanafunzi.

Kwa upande wake, Mhaddhiri wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere-Zanzibar, Dk. Venance Kalumanga, alisema mbali na kujifunza, wanafunzi wanaweza kutumia mtandao kujiendeleza kibiashara ili kuepukana na tatizo la ajira baada ya kuhitimu.



Mtaalamu wa masuala ya mitandao, Dk. Venance Kalumanga ambaye ni Mhadhiri wa Chuo cha Mwalimu Nyerere - Zanzibar, akitoa mafunzo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu juu ya umuhimu wa mtandao wa 4G katika kujiendeleza kielimu na kibiashara wakati wa warsha iliyoandaliwa na Kampuni ya Mawasiliano ya Zantel kujadili matumizi ya 4G kwenye sekta ya elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi matatani tuhuma wizi taa za barabarani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI wa kidato cha nne na cha pili ni miongoni mwa watuhumiwa 11 wanaoshikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za wizi wa nyaya za taa za barabarani.

Nyaya hizo zilizoibiwa zimetolewa katika taa za barabarani zilizowekwa na serikali katika barabara mbalimbali katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mwembe Madema, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Awadhi Haji Juma, alisema kati ya watuhumiwa hao 11, wawili ni wanafunzi waliochini ya umri wa miaka 18 (majina yanahifadhiwa).

Alimtaja mwanafunzi mwingine ni Salum Khamis Ali (18) wa kidato cha nne Shule ya High Perfomance Mwanakwerekwe na mkazi wa Seteni Mjini Unguja.

Watuhumiwa wengine ni ndugu wa familia moja ambao ni Mohamed Khamis Ali (27) na Makame Khamis Ali (19) wakazi wa Chumbuni.

Alisema Julai 29, mwaka huu majira ya saa 8:30 usiku maeneo ya Kibweni karibu na Makao makuu ya Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), walikamatwa watuhumiwa wawili ambao pia ni familia moja wakiwa wamefanikiwa kukata nyaya katika nguzo za barabara kuu kutoka Bububu Mjini wakiwa na vifaa wanavyotumia kufanyia uhalifu huo.

Akiwataja watuhumiwa hao kuwa ni Juma Ali Juma (23) na Fadhili Ali Juma (19), wote wavuvi na wakazi wa Mahonda, Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja.

Alisema baada ya kukamatwa watuhumiwa hao waliwataja watu wanaowapelekea kuwauzia nyaya hizo ambao ni wafanyabiashara wa vyuma chakavu.

Alisema Jeshi la Polisi lilifanikiwa kufika katika ghala hilo na kuwakamata watuhumiwa watano wanaojihusisha na ununuzi wa nyaya hizo na kukamata jumla ya kilo 4,720 za nyaya walizokua wamezihifadhi.

Aliwataja watuhumiwa hao Ajuwedi Juma Ajuwedi (30) mkazi wa Mwera aliyekamatwa na kilogramu 82 za nyaya, Ramadhan Riziki Abdallah (36), mkazi wa Amani aliyekamatwa na kilogramu 26 za nyaya.

Alisema kati ya watuhumiwa hao, watatu walikutwa katika katika ghala la Kampuni ya Zanzibar Steel Co. Ltd lililopo eneo la Kwamchina Wilaya ya Magharibi 'B" Unguja wakiwa na kilo 4,613 za nyaya.

Watuhumiwa ni Mikidadi Hamdu (48), mkazi wa Mpendae, ambaye ni mmiliki wa ghala hilo, Rida Khalifeh Hussein (28), mkazi wa Mbweni ambaye ni Meneja wa ghala na Amin Said Saleh (38), mkazi wa Tomondo, msimamizi wa ghala hilo.

Alisema kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea na utakapokamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Alisema watuhumiwa hao wameisababishia hasara kubwa serikali kutokana na nyaya kugharimu jumla ya Sh. milioni 800.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Polot Energies, S.L.P. 196, Morogoro. | Kiwanja Na. 37, Kitalu "I", Eneo la Uwanja wa ndege, Wilaya ya Morogoro, Mkoa wa Morogoro. | Evans Mella (Mtanzania) | Leseni ya kuhifadhi mafuta (Storage) |
| 2. | Galaxy Auto Center Limited, S.L.P. 1101, Arusha. | Eneo la Moshono, Wilaya ya Arusha Mjini, Mkoa wa Arusha. | Irfhan Virjee (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi (Lubricant) |
| 3. | UK Holding Company Limited, S.L.P. 3215, Dar es Salaam. | Eneo la Chang'ombe, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | John Msigwa (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi (Lubricant) |
| 4. | General Petroleum Limited, S.L.P. 106132, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 289-290, eneo la Chang'ombe, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Irfan Ullah Khan (Mtanzania) | Leseni ya kiwanda cha kutengenezaji vilainishi (Lubricant Blending Plant) |
| 5. | Mount Meru Petroleum Ltd- Buhongwa, S.L.P. 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 8, Kitalu "K", eneo la Buhongwa, Jijini Mwanza. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Liputa Service Station, S.L.P. 45, Mtwara. | Kijiji cha Nagaga, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara. | Karim Liputa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Petroafrica-Mkuti Service Station, S.L.P. 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 205 & 206, Eneo la Mkuti, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara. | Yassin Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 8. | Karim Liputa, S.L.P. 45, Mtwara. | Kijiji cha Chiungutwa, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara. | Karim Liputa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Lake Oil Samora Avenue Dar es Salaam, S.L.P. 5055, Dar es Salaam, | Kiwanja Na. 768/39, Eneo la Samora Avenue, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Oryx Morocco Service Station, S.L.P. 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 27, Eneo la Ursino Estate, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | ABIDA Investment Co. Ltd, S.L.P. 84, Kahama. | Kiwanja Na. 58, Kitalu "A", eneo la Kahama Mjini, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga. | Bakari Juma Nzagamba (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 12. | Katoro Oil, S.L.P 627, Bukoba. | Kiwanja Na. 345, Kitalu "B", eneo la Kagondo, Wilaya ya Bukoba, Mkoa wa Kagera. | Rajesh Prabhudas Ukabhai (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 13. | Valeriani John Ottaru S.L.P 403, Bunda. | Mtaa wa Baiskeli -Bunda Mjini, Wilaya ya Bunda, Mkoani Mara. | Valeriani John Ottaru (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |

**Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

216389002

## RIPOTI MAALUM - V

# Mauaji wivu wa mapenzi yanavyoacha simanzi

**Na Maulid Mmbaga**

**SEHEMU ya nne ya ripoti hii iliendelea kuonyesha matukio mbalimbali ya mauaji yaliyotokea mwaka huu hadi Julai na sehemu kubwa yalichagizwa na wivu wa mapenzi. Endelea sehemu ya mwisho...**



Aprili 26, mtoto wa kike mwenye umri wa miaka mitano, mkazi wa Bukoba vijijini aliomba msaada baada ya kudaiwa kubakwa na babu yake.

Mei 2, mkazi wa kijiji cha Naunambe, wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, Ally Chikukuru (21) alihukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumbaka mama yake mzazi wa miaka 55.

Mei 3, Peter Elias mkazi wa Ndembezi mkoani Shinyanga, alituhumiwa kumuua mke wake Pili Luhende, kwa madai ya kutumia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (ARV) kwa siri.

Mai 5, Elias Mollel (34) mkazi wa Arumeru mkoani Arusha, alituhumiwa kumuua kukatili mke wake Neema Gasper, kwa kumchinja shingo kisha na yeye kujiua kwa kutumia sumu ya panya sababu ni wivu wa mapenzi.

Mei 13, Said Nanguwili (49) mkazi wa Kilwa mkoani Lindi, alishikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mke wake Rafa Omari (40) kwa kile kilichoelezwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Mei 23, Liberatus Mkomed (40), mkazi wa Kibondo mkoani Kigoma alidaiwa kumuawa na askari wa jeshi la akiba kwa kupigwa na fimbo ya chuma sehemu mbalimbali mwilini, baada ya askari hao kumkuta akigombana na mkewe Scholastica Bakunda.

Mei 25, kijana Danieli Manga alishikiliwa na polisi mkoa Mbeya kwa tuhuma za kumuua baba yake Victor Manga (79) kwa kumcharanga mapanga, kwa madai ya kumtuhumu kuwa ni mchawi.

Juni 3, polisi mkoani Iringa lilimshikilia Prudence Patrick (22) kwa tuhuma za kumuua mpenzi wake Petronila Mwanisawa (21) kwa madai ya kutomlipa fedha alizomkopesha kiasi cha Sh. 5,000.

Juni 9, mkoani Dar es Salaam mfanyakazi wa ndani (House boy) Shadrack Kapanga (34), alishikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuwaua mama na watoto wawili na kuiba.

Juni 12, kijana ambaye jina lake halikubainishwa mkazi wa Zanzibar alinusurika kifo baada ya kukutwa akimbaka mtoto mwenye umri wa miaka 10.

Juni 18, mkoani Dodoma, dereva wa daladala aliyefahamika kwa jina moja Hussein alidaiwa kumuua kondakta Juma Hamisi (25) kwa kumpiga na jiwe kisogoni, kwa madai ya kugombea abiria katika kituo cha daladala cha Chang'ombe mkoani hapo.

Juni 19, mkoani Arusha msichana wa kazi za ndani ambaye jina lake halikubainishwa alituhumiwa kumnyonga mtoto wa mwaka mmoja kwa madai yaliyohusishwa na nguvu za giza.

Juni 22, polisi mkoani Mbeya lilimshikilia kijana kwa tuhuma za kumuuwa shangazi yake Lamina Samwebe (65), kwa kumcharanga na mapanga, akimtuhumu kuwa ni mchawi na alikuwa akimloga asipate maendeleo.

Juni 25, Steven Hyera (50), mkazi wa Ruvuma aliyesadikiwa kuwa ni jambazi aliuawa na wananchi wenye hasira kali, kwa tuhuma za kumuua na kumzika ndani ya nyumba yake ofisa mstaafu wa utamaduni wilaya ya Mbinga, Ditrick Mahundi (76).

Juni 28, Adamu Selema (46) mkazi wa mkoa wa Ruvuma alifariki dunia kwa kujinyonga baada ya kumuua mkewe Mwanabibi Mohammed (41) chanzo kikitajwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Julai 3, Muweza Abeid (29) alituhumiwa kwa kumchoma moto na kumjeruhi mwanae wa miaka minne kwa madai ya kula ugali nyama wa bibi yake.

Julai 2, polisi mkoani Kagera liliwashikilia watu wanne kwa tuhuma za kumteka na kumuua kisha kumtupa ndani ya mto Ngono, David James (38), kwa madai kuwa marehemu aliwasaliti kwa kutoa siri za matukio ya wizi.

Julai 4, polisi liliwashikilia watu watano kwa tuhuma za kumuua Badagala Vita (26) kwa kumcharanga mapanga baada ya kumkuta mama yake mzazi akifanya mapenzi na mwanaume mwingine.

Julai 5, mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule moja ya sekondari mkoani Kilimanjaro, alituhumiwa kumnyonga mama yake mzazi hadi kufa kwa madai ya kumpeleka kwa manabii wa uongo kutafuta uponyaji.

Julai 9, polisi mkoani Tabora liliwashikilia watu wanne wanaodhaniwa kuwa ni wezi wa mifugo, kwa tuhuma za kuwaua kwa kuwachinja kikatili watoto wawili wenye umri kati ya miaka 10 na 12, wakiwa machungani na kupora ng'ombe wanne.

Julai 14, mkazi wa Sumbawanga mkoani Rukwa, Alon Cardius (27), aliuawa na wananchi wenye hasira kali baada ya kutuhumiwa kumuua mtoto wake Julai 13 kwa kumkata mapanga ili kumshinikiza mke arudi nyumbani.

Siku hiyo hiyo mkoani Arusha, polisi lilimshikilia kwa mahojiano askari wa jeshi la wananchi wilayani Monduli kwa tuhuma za kumuua Lais Lemomo, wakati akichunga eneo lililokuwa na mgogoro kati ya wafugaji na jeshi.

Julai 16, Grace Mushi (25), alidaiwa kumuua Khamis Abdallah (25) maarufu kama Zungu, mkazi wa Mbezi Makabe kwa kuchoma nyumba moto kwa kutumia mafuta ya petroli kisa wivu wa mapenzi.

Julai 17, Mtu mmoja aitwaye Alex Oraa maarufu kama Simba, alimuua mtu aliyefahamika kwa jina moja la Gift kwa kumiminia risasi tatu mguuni, tumboni na kichwani naye kujipiga risasi ya chini ya kidevu wakiwa baa eneo la Sinza, Dar es Salaam.

Julai 19, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Namtumbo, mkoani Ruvuma miaka 15, alifariki dunia kutokana na kilichodaiwa kuchapwa viboko na mwalimu wake baada ya kufeli mtihani wa majaribio (mock).


IN THE RESDENT MAGISTRATE COURT OF DODOMA
AT DODOMA

EXTENDED JURISDICTION

SENIOR/PRM LAND APPEAL NO 3 OF 2021

(Arising from Land Application No 27 of 2019 of KONDOA District Land and Housing Tribunal for KONDOA)

RAMADHANI SALUM TWAJA...................... APPELLAMT/APP
(Administrator of the Estate of Late TWAJA HUTA MWINJO)

VERSUS

ISSA MSURI KILOMO & 8 OTHERS ......................RESPONDENT

TO 1. AMINA SALUMU DUDU
2. FATUMA KIJENGELILE OF KONDOA.

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION.

**TAKE NOTICE** that the above case been fixed for hearing/mention on 6th day of AUGUST 2021 at 09:00AM.
Before **HON D.J. MPELEMBWA SRM.**
**YOU ARE** required to appear in this Court on the fixed date without fail. And you may bring with you are all required documents in support of your case.

**Given under my hand and seal of the Court this 14th day of JULY 2021.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
COPY TO BE SERVED UPON

116388501



# Loftus-Cheek awekwa mtegoni

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema anataka kuona Ruben Loftus-Cheek anafanya kazi kwa asilimia 150 kama anataka kujihakikishia nafasi ya kukaa kwa muda mrefu hapo Stamford Bridge.

Loftus-Cheek amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu England, huku Lazio ikiripotiwa kuwania saini yake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, ambaye amekuwa na Chelsea tangu akiwa na umri wa miaka nane, alitumia msimu uliopita kucheza kwa mkopo kule Fulham, akicheza mechi 32 katika mashindano yote.

Akiwa amechukua nafasi ya kocha Frank Lampard Januari, mwaka huu, kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya yamemfanya Tuchel kufanya kazi na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye amecheza katika mechi mbili za kirafiki dhidi ya Bournemouth na Arsenal.

Ingawa alisifia kiwango cha Loftus-Cheek, raia huyo wa Ujerumani ana matumaini mchezaji huyo anaweza kujaribu kufanya vizuri ili kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza.

"Ni mapema mno kumhukumu Ruben," alisema Tuchel. "Ana kila kitu mikononi mwake na ni suala lake kuamua kuhusu majaliwa yake kama mchezaji.

"Anatakiwa kufanya kazi kwa asilimia 150 kwa sababu asilimia 100 hazitoshi."

# UNITED MATUMAINI KIBAO KWA HALAAND

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United wameripotiwa wana matumaini kuwa mkataba mpya wa kocha wao, Ole Gunnar Solskjaer pale Old Trafford utawaweka kwenye nafasi nzuri ya kupambana ili kumnasa Erling Braut Haaland msimu ujao wa majira ya joto.

Nyota huyo raia wa Norway anatarajiwa atatumia msimu mzima pale Borussia Dortmund kabla ya kuondoka mwakani kukiwa na dau la pauni milioni 68 kwenye mkataba wake.

Chelsea, Barcelona, Real Madrid na Manchester City waote wanaweza kuwania huduma ya Haaland mwaka 2022, lakini kwa mujibu wa Daily Star, matumaini ya Man United kwenye dili hili yanapewa nguvu na mkataba mpya wa Solsjaer.

Bosi huyo mwenye umri wa miaka 48 amesaini mkataba mpya wa miaka mitatu na United na ana uhusiano wa muda mrefu na Haaland baada ya kuwa naye zamani kwenye kikosi cha Molde.

Haaland amefunga magoli 57 kwenye mechi 59 za Dortmund tangu kuwasili kwake mwaka 2020.



# Mbappe kuwaondoa nyota Madrid

**MADRID, Hispania**

BAADA ya kuwaachia Sergio Ramos na Raphael Varane waondoke, Real Madrid inaripotiwa kwa sasa, Thibaut Courtois, Karim Benzema, Fede Valverde, David Alaba na Vinicius ndiyo wachezaji pekee ambao haitawagusa.

Ukiachana na Courtois, Benzema, Valverde, Alaba na Vinicius, kila mchezaji wa kikosi hicho cha kocha, Carlo Ancelotti wapo sokoni.

Real Madrid wapo tayari kuwauza asilimia kubwa ya wachezaji wao ili wapate fedha za kufadhili uhamisho wa Kylian Mbappe kutoka kule PSG.

Klabu haina mpango wa kuingia sokoni kusajili mchezaji mwingine wa kati, kwa mujibu wa Football Hispania watawekeza kwenye kuweka sawa mikataba ya Alaba, Nacho na Eder Militao.

Real wamepania hawatasajili mchezaji mwingine yeyote kwenye dirisha hili la uhamisho isipokuwa Mbappe.

Mfaransa huyo amekuwa akiwaniwa kwa muda mrefu na Madrid na sasa wanaonyesha kuwa makini kuhakikisha dili hilo linakamilika. Na watawauza wachezaji watakaopata ofa zao hadi mwisho wa Agosti kwa ajili ya kukamilisha suala hilo.

Real Madrid inapata nguvu kubwa kwenye mbio zake za kuwania kumsajili Mbappe, baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa kukataa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, huku wa sasa ukiwa unamalizika mwakani.



## HABARI MICHEZO



# BARCA:

## GRIEZMANN, COUTINHO HAWAUZWI

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imeripotiwa kubadilisha mipango yao juu ya kuwauza Antoine Griezmann na Philippe Countinho na sasa wamepanga kubakia na wachezaji hao kwa ajili ya msimu huu mpya.

Wachezaji hawa wote wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo wakati Barcelona wakijaribu kuweka sawa matatizo yao ya kifedha.

Kwa mujibu wa Mundo Deportivo, tayari kuliripotiwa nia kutoka klabu za Ligi Kuu England za kuwawania kuwasajili wachezaji hao, lakini Barcelona wameamua hakuna atayeondoka hapo Camp Nou.

Ripoti zinasema kocha mkuu Ronald Koeman anataka wachezaji hao wawili waendelee kuunda kikosi chake cha kwanza msimu ujao na itakuwa hivyo labda yatokee mabadiliko yanayoweza kuathiri upatikanaji wa mchezaji yeyote kati yao.

Barcelona wameongeza nguvu kwenye safu yao ya ushambuliaji baada ya kuwasili kwa Sergio Aguero na Memphis Depay bure, huku Lionel Messi akiwa bado hajasaini rasmi mkataba mpya klabuni hapo.

Vijana hao wa Koeman, wanajiandaa kupambana kwa ajili ya msimu mpya, na watafungua mbio zao za ligi kwa mechi dhidi ya Real Sociedad Agosti 15, mwaka huu.

## RODRIGUEZ AFUNGUKA HAJUI ATAKAPOCHEZA

**LONDON, England**

JAMES Rodriguez hajawahi kuwa nje ya vichwa vya habari msimu huu wa joto na hatima ya mchezaji huyo wa Everton na Timu ya Taifa ya Colombia hadi sasa haijulikani.

Baada ya kuachwa kwake kwenye kikosi cha Colombia kilichocheza michuano ya Copa America 2021 msimu huu wa joto, mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid, ameuliza maswali juu ya wapi atacheza mpira wake msimu ujao.

"Nimecheza tayari kwenye ligi zote," alisema nyota huyo akinukuliwa na Daily Mail.

"Nimebaki na Italia tu. Itakuwa vizuri kucheza huko na kuwa na rekodi hiyo, lakini sijui kama itatokea siku za usoni."

Miamba ya Serie A AC Milan inaripotiwa kuwa na hamu ya kumsajili James msimu huu wa joto na yeye mwenyewe amekiri kuwa hajui atacheza wapi msimu ujao, ingawa amesema kwamba hajioni akirudi Real Madrid.



"Sijui kabisa nitacheza wapi. Ni mada ngumu sana. Wacha tuone ni nini kitatokea. Sitaki kusema ndio au hapana kwa sababu sijui nini kitatokea. Ninafanya mazoezi vizuri.

"Kwenye mpira wa miguu haujui nini kitatokea. Ninajua tu kuwa ninafanya mazoezi vizuri na ninafanya kazi kwa bidii, nikifikiria juu ya sasa. Ninafanya mazoezi kwa bidii kwa kile kitakachokuja."

# TRAORE ANUKIA KUSAJILIWA LEEDS

**LONDON, England**

KLABU ya Leeds United inamwangalia winga wa Wolves, Adama Traore kama mchezaji muhimu wanayetaka kumsajili katika majira haya ya kipindi cha joto ili kuongoza nguvu kwenye kikosi chao.

Mazungumzo ya mkataba mpya kati ya winga huyo wa Hispania na klabu yake yamekwama, na kuvutia wapinzani wao hao wa Ligi Kuu England.

Leeds wanahitaji kujiimarisha kuelekea katika msimu mpya wa 2021/22 na kukamilisha saini ya Traore kunaweza kuwagharimu pauni milioni 30 kuwashawishi Wolves.

Traore bado ana mkataba na Wolves mpaka mwaka 2023 hivyo klabu hiyo bado wana nafasi ya kumbakisha mchezaji huyo, lakini wanaweza kubadili uamuzi wao endapo ofa nzuri kuanzia pauni milioni 30 itapelekwa.

Leeds pia inakabiliwa na upinzani kutoka katika vilabu mbalimbali ikiwamo Liverpool, Chelsea na Barcelona ambao wamewahi kuhusishwa na mchezaji huyo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GREALISH AKARIBIA KUACHANA NA VILLA

## ●●● Ni kutokana na ofa nono iliyowekwa mezani na Manchester City huku...

**LONDON,** England

JACK Grealish amerudi kutoka mapumziko na jana Jumatatu alifanya mazungumzo na Aston Villa kuhusu hatima yake wakati akihusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester City, kwa mujibu wa The Mirror.

Grealish alichukua likizo baada ya michuano ya Euro 2020, na sasa anatarajiwa kutoa uamuzi kuhusu majaliwa yake ya baadaye.

Uvumi kwa muda mrefu umebainisha Manchester City wamevutiwa sana na Grealish, huku kocha wake, Pep Guardiola akitajwa kuwa shabiki wake mkubwa.

Mapema wiki iliyopita, Aston Villa waliripotiwa wako tayari kukubali ombi la Manchester City la pauni milioni 100.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wanaaminika kuwasilisha ofa kubwa Ijumaa iliyopita, huku wakifanya mazungumzo ya moja kwa moja na Aston Villa juu ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

Ripoti ya Sky Sports, ilisema kikosi hicho cha kocha Dean Smith bado kina nia ya kumshikilia mchezaji huyo na wameweka mezani mkataba mpya ulioboreshwa zaidi wakiamini nyota huyo atazingatia kusalia klabuni hapo.

Ofa ya mkataba mpya imeboreshwa maslahi na inatajwa endapo atasaini mkataba mpya, atalipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki.

Hata hivyo, ripoti zinadai Aston Villa wako tayari kukubali ofa ya City ya pauni milioni 100, ikimaanisha kuwa itakuwa ni juu ya Grealish kuamua kama anataka kuhamia katika klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alifunga mabao saba na kuchangia asisti 12 katika mechi 27 kwenye za Aston Villa kwa msimu wa 2020-21, huku akitoa mchango kwenye mechi tano za Euro 2020.

Bosi wa City, Guardiola anadaiwa anatamani saini ya Grealish ipatikane kabla ya kikosi chake kuingia dimbani kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Leicester City hapo Agosti 7, mwaka huu.

## KWA UFUPI

### CITY KUMTOSA KANE

MANCHESTER City wataachana na mipango ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, endapo watafanikiwa kumnasa nyota wa Aston Villa, Jack Grealish mwenye miaka 25. (***Manchester Evening News***)

### RODRIGUEZ NJIA MOJA

KIUNGO Colombia, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 30, ameelezwa hayupo kwenye mipango ya kocha mpya wa Everton, Rafael Benitez, na kwamba yupo huru kuhama klabuni hapo endapo ofa nzuri itawasilishwa. (***Liverpool Echo***)

### MARTINEZ ANUKIA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid imepiga hatua moja mbele ya Arsenal katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez ambaye ana thamani ya Euro milioni 90. (***Tuttosport***)

### ROMERO SAFI SPURS

OFA ya pauni milioni 43 iliyotolewa na klabu ya Tottenham Hotspur kutaka kumsajili beki wa Argentina, Cristian Romero imekubaliwa na klabu ya Atalanta. (***Talksport***)

### TRAORE KUTUA LEEDS

LEEDS United wapo katika mipango ya kutaka kumsajili winga wa Hispania anayechezea klabu ya Wolves, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25, ambaye anakadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 30. (***Goal***)

### NUNO AMGEUKIA TRAORE

KLABU ya Tottenham Hotspur ambayo sasa inanolewa na kocha wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo pia inapiga hesabu za kutaka kumsajili Adama Traore. (***Mail***)

### ZOUMA AWANIWA WEST

KLABU ya West Ham ipo kwenye mazungumzo na klabu ya Chelsea juu ya usajili wa beki wa kati raia wa Ufaransa, Kurt Zouma mwenye umri wa miaka 26. (***Sun***)

### MILENKOVIC SOKONI

IWAPO West Ham watashindwa kumsajili Kurt Zouma kutoka Chelsea, basi mbadala wake wanapanga awe beki raia wa Serbia, Nikola Milenkovic anayechezea klabu ya Fiorentina. (***Sky Sport***)

### PALACE YAJIPANGA

KLABU ya Crystal Palace inataka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji kutoka England, Ademola Lookman (23), anayechezea katika klabu ya RB Leipzig. Mipango ya Palace hata hivyo huenda ikakumbana na upinzani kutoka Burnley na Watford. (***Sun***)

### SANCHEZ ANUKIA SEVILLA

WAKALA wa beki wa Tottenham Hotspur, Davinson Sanchez (25), amefanya mazungumzo na Sevilla ili beki huyo kuhamia katika klabu hiyo. Sanchez raia wa Colombia amekuwa akinyemelewa na Sevilla ili kuchukua nafasi ya Jules Kounde (22), ambaye amekuwa akihusishwa na mipango ya kuhamia Chelsea. (***Caracol Radio via Mail***)

### RAMSEY AIKATAA WOLVES

KLABU ya Wolves imeweka wazi nia yake ya kutaka kumsajili kiungo wa Wales, Aaron Ramsey kutoka miamba ya Italia Juventus, hata hivyo kiungo huyo wa zamani wa Arsenal mwenye miaka 30 anaripotiwa kutoshawishika na ofa hiyo. (***Calciomercato - Italian***)

**HABARI MICHEZO**

# NAMUNGO KAMILI KUMSAJILI MIRAJI, YAMWACHA ABAROLA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Miraji Athuman 'Sheva', ameingia katika rada za kutakiwa na Namungo FC ambayo inahitaji kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa 2021/2022, imefahamika.

Sheva ambaye amemaliza mkataba na Simba, ni miongoni mwa nyota ambao wameshindwa kupata nafasi katika kikosi cha kwanza cha Wekundu wa Msimbazi ambacho msimu uliomalizika kilifanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili jijini jana kutoka ndani ya timu hiyo zinasema mazungumzo baina ya pande hizo mbili yanaendelea vizuri wakati wowote anatarajia kuingia mkataba na timu hiyo ya mkoani Lindi.

Chanzo hicho kilisema usajili wa Sheva ni mapendekezo ya benchi lao la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Hemed Morocco ambaye ameainisha nafasi na majina ya wachezaji ambao anaowahitaji kwa kuelekea msimu mpya.

"Ni kweli tuko na mazungumzo na Sheva, hilo linafanyika kwa sababu liko katika moja ya mapendekezo ya kocha kwenye nafasi ya ushambuliaji ambayo anahitaji nyota wapya wawili, tunatarajia kupata huduma wa nyota huyo kwa sababu ni huru baada ya mkataba wake na Simba ukifikia ukingoni," alisema kigogo huyo.

Aliongeza katika ripoti hiyo wanatarajia pia kuachana na golikipa wao namba mbili, Nurdini Abarola ambaye amemaliza mkataba na sasa wanahitaji kusajili mlinda mlango mzawa.

Gazeti hili lilimtafuta Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Selemani alisema wanafanyia kazi ripoti ya kocha wao kwa sababu wanahitaji kufanya vizuri katika msimu huo mpya.

Selemani alizitaja nafasi ambazo wanatakiwa kufanyia kazi ni pamoja na ya ushambuliaji, kiungo mshambuliaji, kiungo wa kati, kiungo mkabaji, beki wa kulia, beki wa kushoto na golikipa.

"Tuko katika mchakato wa kuzungumza na wachezaji wapya na waliomaliza mkataba na wako katika mapendekezo ya kocha, suala la nani atasajiliwa litakuja hapo baadaye tutakapomalizana na nyota ambao wamependekezwa," alisema katibu huyo.

Aliongeza kikosi chao kitaanza maandalizi ya msimu mpya mapema kwa sababu wanahitaji kuanza vizuri Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.



Wachezaji wa Yanga wakishangilia baada ya straika wao, Waziri Junior kufunga bao katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Kombe la Kagame dhidi ya Nyasa Big Bullets iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMKM yaahidi makubwa Kagame Cup

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wamewasili salama jijini Dar es Salaam na kutamba wamejiandaa kufanya vyema katika mashindano ya Kombe la Kagame yanayoendelea hapa nchini.

KMKM ambayo imepangwa Kundi A na jana jioni ilianza kutupa karata yake kwa kucheza dhidi ya Le Messager Ngozi kutoka Burundi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu alisema wamejiandaa kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa sababu wana 'kiu' ya kutwaa ubingwa wa kombe hilo mwaka huu.

Msimu alisema wamepata muda mrefu wa maandalizi ya timu yao, hivyo wanatarajia wachezaji wataonyesha kile walichofundishwa na hatimaye kuipa heshima Zanzibar.

"Tumejiandaa kushinda, tumepata muda mwingi wa kufanya mazoezi na kucheza mechi mbalimbali za kirafiki, kwetu sisi kila mashindano yana umuhimu mkubwa kwa kuwa tupo katika maandalizi mengine ya kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Msimu.

Aliongeza katika mashindano hayo atamkosa mshambuliaji wake tegemeo, Mussa Ali Mbarouk ambaye alipata majeraha katika michezo ya lala salama ya Ligi Kuu Zanzibar.

"Hata hivyo tumemwongeza mchezaji mpya, Mwinyi Haji Ngwali ili kuhakikisha lengo la kuchukua ubingwa michuano hiyo linatimia," Msimu alisema.

## Azam FC yatamba itaendelea kusajili

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kusajili wachezaji sita mpaka sasa, Azam FC imesema bado inaendelea na usajili wa wachezaji wapya kwa ajili ya msimu ujao Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa, huku ikitarajia kutambulisha wengine leo au kesho.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, alisema bado wanaendelea kusajili wachezaji wa nje na wa ndani ili kukijenga kikosi chao ambacho msimu ujao kitashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kuna watu wanaona kama eti tumemaliza. Kwenye michuano ya kimataifa tunaweza kusajili hadi wachezaji 40. Tuliona hata msimu uliopita, CAF waliruhusu timu kusajili hadi wachezaji 40, kwa nini kwetu iwe ajabu kuendelea kusajili?" Alihoji Zacharia.

Mpaka sasa Azam imewasajili wachezaji Idris Mbombo kutoka El Gouna ya Misri, Rodgers Kola, Charles Zulu, Paul Katema na Kenneth Muguna na Edward Manyama kutoka Ruvu Shooting.

Kuhusu michuano ya Kombe la Kagame, Zacharia alisema wanawatumia wachezaji ambao hawakupata muda wa kutosha kwenye Ligi Kuu Bara na Kombe la FA msimu uliomalizika, baadhi ya wachezaji wa timu ya vijana, pamoja na wachezaji waliorejea klabuni baada ya kumaliza kutumikia klabu nyingine kwa mkopo.

"Kuna baadhi ya wachezaji wetu ambao tuliwatoa kwenye klabu mbalimbali kwa mkopo, tumewarudisha na hao watatumika kwenye michuano ya Kagame," alisema kiongozi huyo.

## Dodoma Jiji FC mambo yatanoga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Dodoma Jiji umesema unatarajia kusajili wachezaji wapya wenye uwezo mzuri kwa ajili ya timu yao kuonyesha ushindani katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Fortunatus Johnson aliliambia gazeti hili tayari wameanza kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi, na hivyo wanaamini msimu mpya watakuwa na kikosi imara.

Johnson alisema jana jioni walitarajia kufanya kikao cha Bodi ya Wakurugenzi na baada ya kumalizika kwa kikao hicho, wataanza utekelezaji mapema.

Alitaja nafasi ambazo wataziboresha ni pamoja na ya golikipa, beki wa kati, kiungo mkabaji na mshambuliaji.

"Tutakutana leo (jana), baada ya hapo sasa tutaanza mchakato wa kujaza nafasi kama tulivyoshauriwa, bado hatujafanya mazungumzo na mchezaji wowote kwa sababu hatukuwahi kukutana na kujadili ripoti ya ufundi," alisema kiongozi huyo.

Michezo
Jumanne Agosti 3, 2021
Nipashe



## Grealish akaribia kuachana na Villa

HABARI UK. 22



Kiungo mpya wa Yanga, Dickson Ambundo (katikati), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Nyasa Bis Bullets ya Malawi katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Kombe la Kagame iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA, YANGA ZAKIMBIZANA

## ●●●Ni katika mbio za usajili kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano ya CAF...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha kila timu inaimarisha makali yake kuelekea msimu mpya wa 2021/22, klabu za Simba na Yanga zote za jijini Dar es Salaam zimeendelea kusajili wachezaji wapya kwa ajili ya kufanya vyema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana jijini jana, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba jana waliingia makubaliano ya miaka mitatu na kiungo mkabaji wa Kagera Sugar, Abdulswamad Kassim 'Guty'.

Chanzo chetu cha habari kilisema Simba ilifikia makubliano na nyota huyo mara baada ya msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumaliza na vile vile ilijiridhisha kwamba ameshaagana na waajiri wake wa zamani.

Akizungumza na Nipashe jana, Guty alithibitisha kumalizana na uongozi wa Simba na kuweka wazi anajisikia furaha kuwa sehemu ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi.

"Ni kweli nimesaini mkataba wa miaka mitatu na Simba, hatua hii ilikamilika baada ya kumaliza mkataba wangu na waajiri wangu wa zamani, Kagera Sugar, nimefurahi kutua Simba na niko tayari kwa ajili ya kuisaidia timu kufikia malengo yake," alisema Guty. Usajili Guty ni kuongeza ufanisi wa nafasi mbalimbali ikiwamo kiungo mkabaji, hasa baada ya kuwapo kwa sintofahamu ya utovu wa nidhamu wa mara kwa mara kwa Jonas Mkude.

Nafasi ya kiungo mkabaji ndani ya Simba kwa sasa ina wachezaji wawili wa asili ambao ni Mzamiru Yassin na Mganda, Taddeo Lwanga.

Nyota wengine ambao wanatajwa tayari wameshamalizana na Simba ni pamoja na Kipa kutoka Tanzania Prisons, Jerimiah Kisubi, beki wa KMC FC, Israel Mwenda na mshambuliaji wa Mbeya City, Dennis Kibu.

Kwa upande wa Yanga ambayo sasa inashiriki mashindano ya kimataifa jana imemtambulisha, Yusuph Athumani kutoka Biashara United ya Musoma mkoani Mara.

"Tunapenda kuwajulisha rasmi kuwa Yusuph Athumani sasa yuko katika jezi ya kijani na njano," ilisema kwa kifupi taarifa iliyotolewa na uongozi wa Yanga.

Mabosi wa Yanga pia wako katika hatua ya mwisho wa kukamilisha mazungumzo na mshambuliaji Mkongomani Heritier Makambo ambaye alitua nchini juzi na moja kwa moja alifika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuitazama timu yake ya zamani ikicheza dhidi ya Big Bullets ya Malawi katika mechi ya Kombe la Kagame iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilishafungua rasmi dirisha la usajili ambalo litafungwa rasmi ifikapo Agosti 31, mwaka huu.

## Upinzani mkali ujumbe wa TFF

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI orodha ya mwisho ya wagombea wanaowania uongozi katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imetangazwa, ushindani umeonekana kutawala zaidi kwenye upande wa nafasi za Ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya shirikisho hilo, imefahamika.

TFF inatarajia kufanya uchaguzi mkuu Jumamosi kwenye Ukumbi wa Hoteli ya Tanga Beach Resort jijini Tanga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Kiomoni Kibamba inasema nafasi ya urais ina mgombea mmoja ambaye ni Wallace Karia, anayetetea cheo hicho.

Taarifa hiyo ilitaja wagombea waliobakia wanaowania ujumbe katika Kanda namba moja yenye kujumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Lindi, Mtwara ni Athumani Kambi, Hossea Lugano 'Maisha' na Lameck Nyambaya wakati Kanda namba mbili wanaochuana ni Khalid Abdallah na Zakayo Mjema.

Kanda namba tatu ambayo itawakilisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Songwe na Njombe wanaogombea ni Abousufian Silia, James Mhagama na Mohammed Mashango huku Kanda namba nne inayoundwa na mikoa ya Dodoma, Singida, Simiyu na Shinyanga wanaopambana ni Mohamed Aden, Osuri Kosuri na Hamisi Kitila.

Salum Chama, Vedastus Lufano na Salum Kulunge wao wanawania ujumbe wa Kanda ya tano inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Geita, Mara na Kagera wakati Kanda namba sita inayowakilisha mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa wanaochuana ni Issa Bukuku, Blassy Kiondo na Keneth Pesambili.

Baada ya uchaguzi huo kumalizika, rais atakuwa na nafasi ya kuteuwa wajumbe wanne watakaoungana kuunda kamati ya utendaji na vile vile kumthibitisha mmoja wao ili kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais.

Katiba ya TFF pia inasema Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake cha Tanzania (TWFA), pia anaingia moja kwa moja katika kamati hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >